# Nipashe

Jumatano Novemba 22, 2023 • Tanzania 1000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581502

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

**ANAYEDAIWA** kumnyonga mtoto sasa kupimwa akili

UKURASA 3



**ZIARA** Samia India yazidi kuibua fursa


UKURASA 5

**HAKIMU** amhoji baba kuruhusu bintiye kushika dawa kulevya

UKURASA 4

# LHRC yaibua hoja 11 sheria uchaguzi

UKURASA 2






## Mwigulu ashtuka makandarasi wa nje kulipwa mabilioni

UKURASA 3

UKURASA WA 24

### SIMBA SC WAREJESHA UMOJA KUIUA ASEC MIMOSAS

BAADA ya Sintofahamu na kutokea mengi ikiwamo mashabiki kuwarushia maneno viongozi, Klabu...

### Wakurugenzi matatani kisa miradi ya maendeleo

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YAIFUATA BELOUIZDAD NA MKAKATI MKALI UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi (wa pili kushoto) na Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Godwell Ole Mening'ataki, wakionyesha kwa waandishi wa habari, mjini Iringa jana, meno ya tembo na silaha mbalimbali za jadi zilizokamatwa kwa watuhumiwa wa ujangili 34. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# LHRC yaibua hoja 11 sheria uchaguzi

**Na Halfani Chusi**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimetoa mapendekezo 11 ya kuboresha miswada mitatu inayosimamia mchakato wa uchaguzi nchini.

Miswada hiyo ni ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Vyama vya Siasa na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, aliweka bayana maoni ya kituo hicho kuhusu miswada hiyo iliyowasilishwa bungeni katika Mkutano wa 13 wa Bunge uliomalizika hivi karibuni, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jana, Dar es Salaam.

Pamoja na uchambuzi uliofanyika, LHRC imetoa mapendekezo ya jumla ambayo pamoja na mambo mengine, ikitaka kujumuishwa haki ya wafungwa kupiga kura kwa utaratibu utakaowekwa kwa sheria kama ilivyoamuliwa na Katiba ifanyiwe marekebisho kuweka mfumo wa usaili wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi.

Pia imependekeza muswada uweke wazi sifa ya wajumbe wa tume kutokuwa na chama cha siasa miaka mitano kabla ya kuteuliwa na Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa ujumuishe kipengele cha kuwapo chombo maalum cha usuluhishi wa migogoro ndani ya vyama.

Katika Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, kiwekwe kifungu cha takwa la kufanyika mdahalo wa kitaifa wa wagombea wote wa nafasi ya urais.

"Mswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Ubunge na Madiwani uweke kifungu kinachotoa haki kwa Watanzania waishio nje ya nchi (diaspora) kuwa na haki ya kupiga kura kwa utaratibu ambao sheria itaweka," alisema.

Dk. Henga alishauri serikali kupitia vikao vya bunge vya Februari, mwakani, iwasilishe muswada wa sheria itakayosimamia uchaguzi wa serikali za mitaa tofauti na ilivyo sasa ambapo Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ndicho chombo chenye jukumu hilo.

Pia alishauri kiongezwe kifungu ndani ya Mswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kitakachoweka utaratibu wa ukaguzi wa daftari la wapigakura kwa kutumia tume na wadau wengine.

"Ni muhimu kiongezwe kifungu ndani ya Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kitakachoruhusu wananchi kujisajili kuwa wapigakura kwa kutumia mfumo wa mawakala.

"Pia kiongezwe kifungu kitakachoweka utaratibu wa kumwajibisha msimamizi wa uchaguzi atakayeharibu au kuvuruga uchaguzi kwa makusudi kwani kifungu cha 138 cha muswada hakijabainisha utaratibu huo pamoja na kuifanya ajenda ya Katiba Mpya iwe endelevu na iguse maeneo muhimu," alisisitiza.

Akifanya uchambuzi wa miswada hiyo, alisema kifungu cha sheria kinachomtaka mpigakura atakapopoteza kitambulisho au kuharibika alipie ada iliyoainishwa na tume ili kupata kingine kifutwe.

Hali hiyo, alisema itachochea wengi waliopoteza au kuharibu vitambulisho vyao kutopiga kura kutokana na kukosa gharama ya kupata kitambulisho kingine kwa sababu ya hali ya maisha ya Watanzania.

Dk. Henga alisema LHRC inapendekeza kufutwa kwa kifungu hicho ili kuwawezesha Watanzania watakaopoteza vitambulisho au kuharibika wapatiwe bure bila masharti yoyote, ili kuwapa fursa ya kutimiza haki yao kikatiba ya kuchagua viongozi kama ilivyo kwa vitambulisho vya taifa ambavyo hutolewa bure.

Pia alimulika upungufu waliobaini kwenye miswaada hiyo ikiwamo mkurugenzi wa uchaguzi kuwa katibu wa kamati ya usaili.

"Sheria imeanzisha kamati ya usaili ambayo kazi yake ni kusaili wajumbe wa tume ya uchaguzi. Kwa mujibu wa kifungu cha 9 (3) cha muswada, Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, atakuwa katibu wa kamati ya usaili inayoanzishwa chini ya kifungu 9(1) cha muswada.

"Kitendo hicho kinaashiria mkanganyiko wa wazi kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha muswada. Mkurugenzi atapatikana kwa kuteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na tume. Swali la msingi linakuwa kipi kinaanza kati ya tume na mkurugenzi wa uchaguzi? Hapa tunarudi kwenye hadithi zile zile kipi kilitangulia kati ya kuku na yai," alisema.

Alitaja upungufu mwingine kuwa ni muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, watumishi wa umma kuendelea kuwa sehemu ya tume, tume kuendelea kutegemea bajeti ya serikali, tume kushauriana na waziri mwenye dhamana na masuala ya utumishi kuandaa muundo wa utumishi wa sekretarieti ya tume.

Pia kigezo cha mtu kuwa ofisa mwandamizi katika utumishi wa umma ili kuteuliwa kuwa mkurugenzi wa uchaguzi, wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kuendelea kuwa wasimamizi wa uchaguzi na uamuzi wa tume kuwa wa mwisho kutopingwa mahakamani.

"Kwa mujibu wa kifungu cha 21 cha muswada, tume itaendelea kutumia au kuazima watumishi wa umma kuwa wasimamizi wa uchaguzi. Kwa lugha nyingine, wakurugenzi wa halmashauri, watendaji wa kata, walimu na watumishi wengine wa serikali wataendelea kuwa sehemu ya wasimamizi wa uchaguzi ingawa neno lililotumika ni kuazima. Ukweli ni kwamba watumishi wa umma wataendelea kuwa sehemu ya tume kinyume cha matarajio ya wengi.

"Kifungu hiki pia kinakiuka uamuzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu katika shauri la LHRC na Bob Chacha Wangwe, dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema.

## Wakurugenzi matatani kisa miradi maendeleo

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

RIPOTI ya awali ya uchunguzi ya timu ya wataalam iliyoundwa kuwachunguza wakurugenzi wawili wa halmashauri nchini, walioshindwa kusimamia miradi ya maendeleo, imewaweka 'matatani'.

Wakurugenzi hao wameingia matatani baada ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa, kuwasimamisha kazi ili kupisha uchunguzi.

Waliosimamishwa kazi kutokana na ripoti hiyo ni Butamo Ndalahwa ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani na Mkurugenzi wa Mji wa Ifakara, Lena Nkaya.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Hosea Nteghenjwa, ilisema Waziri Mchengerwa amewasimamisha kazi wakurugenzi hao kuanzia Novemba 20, mwaka huu.

Sehemu ya taarifa hiyo ilisema Waziri Mchengerwa amechukua hatua hiyo baada ya kupokea taarifa ya awali ya timu iliyoundwa kuchunguza tuhuma za wakurugenzi hao kushindwa kusimamia miradi ya maendeleo kwenye halmashauri zao kwa nyakati tofauti.

Timu hiyo iliyoundwa na Katibu Mkuu, kwa maelekezo ya Waziri Mchengerwa imebaini upungufu ikiwamo kushindwa kusimamia miradi ya maendeleo.

Waziri Mchengerwa amewasimamisha kazi kwa kuzingatia Kanuni ya 37 (1) na 38 (1) ya Kanuni za Watumishi wa Umma za Mwaka 2022 ili kupisha uchunguzi wa kina.

Aidha, amewasisitiza Wakurugenzi wote wa mamlaka za serikali za mitaa kutekeleza majukumu yao kikamilifu ikiwamo kusimamia miradi ya maendeleo.

Pia Waziri huyo wa TAMISEMI, ameendelea kusisitiza kuwa hatasita kuchukua hatua stahiki kwa atakayethibitika kutenda kinyume.

Rais Samia Suluhu Hassan alimteua Butamo Ndalahwa kuwa DED Kibaha na Lena Nkaaya kuwa Mkurugenzi wa Mji wa Ifakara Agosti 1, mwaka 2021.

**HABARI KITAIFA**

# Mwigulu ashtuka makusanyo kodi kulipwa makandarasi wa kigeni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema licha ya serikali kukusanya kodi katika mazingira magumu, kiasi kikubwa cha fedha hizo kinakwenda nje ya nchi kwa kulipa kampuni za makandarasi wageni wa ujenzi wa miradi mingi nchini.

Dk. Mwigulu, alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akifungua mkutano wa makandarasi na washauri elekezi wazawa wenye lengo la kujadili nafasi yao katika utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini.

"Inatuumiza sana pesa nyingi zinakwenda nje tunakusanya kodi za wananchi kwa shida sana, lakini kiasi chote kinakwenda kunufaisha wengine na hawa makandarasi wageni tunalipa kwa dola, lakini pia ukichelewa tu hata nusu saa kulipa unatozwa riba.

"Huwa inaniuma sana pale unapokuta serikali mnapigwa presha na kampuni hizi kwa ajili ya malipo yao na wakati mwingine unakuta huyo mkandarasi nchi yake haijawahi kutoa hata mkopo kwa taifa letu, lakini kampuni zake zimetekeleza miradi ya zaidi ya trilioni 70," alisema.

Pia, katika kipindi kifupi cha uongozi wa serikali ya awamu ya sita, serikali imetekeleza miradi mingi ambayo imetumia kiasi kikubwa cha fedha.

Alisema pamoja na serikali kutumia kiasi kikubwa cha fedha kutekeleza miradi hiyo, mingi imekwenda katika kampuni za makandarasi ya wageni.

Mwigulu alisema, kutokana na hali hiyo serikali inapaswa kuwezesha kampuni za makandarasi wazawa ili wawe na uwezo wa kushindana na wageni ili fedha zote zinazotolewa zibaki nyumbani.

"Kama leo hii kuna wataalam ambao wamesoma na kuwa na uwezo wa kupandikiza figo wagonjwa hapa nchini, lakini pia wapo wanaoweza kupandikiza uloto ndani ya nchi, kwanini mainjia wetu tangu uhuru hadi sasa wasiwe na uwezo wa kujenga hata daraja tu tena siyo la mto ni mfereji tu," alihoji Dk. Nchemba.

Aidha, alisema kikao hicho ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuwajengea uwezo makandarasi wazawa ili kuwa na uwezo wa kutekeleza miradi yote nchini bila kutegemea wageni.

"Katika mkutano huu leo hapa tutajadili yote yanayotukwamisha kushindwa kufika ili kila mmoja wetu akiondoka hapa aondoke na kitu cha kwenda kufanyia kazi ili hizi fedha zote tubaki nazo sisi na hawa wageni siye ndio tuwaajiri siyo wao kutuajiri sisi," alisema.



Akizungumzia malipo ya makandarasi wazawa ambayo yanalalamikiwa katika maeneo mengi chini, alisema mpango ulipo ni kuongeza bajeti ili kumaliza tatizo hilo.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alisema tathmini ya jumla inaonesha kuwa ingawa idadi ya miradi iliyotekelezwa na makandarasi wazawa ni asilimia 96 ya miradi yote iliyosajiliwa na CRB, thamani ni asilimia 38.5 pekee ya miradi yote iliyosajiliwa.

"Kwa ulinganifu wa idadi ya makandarasi wazawa waliosajiliwa na CRB, tathmini inaonesha kwamba, kampuni zenye sifa za wazawa ni 14,000 sawa na asilimia 94.6 wakati zenye sifa za wageni ni 800 sawa na asilimia 5.4 tu," alisema Bashungwa.

Hiyo inamaanisha kuwa makandarasi wa nje ambao ni wachache kwa idadi ya asilimia 5.4 wanatekeleza miradi michache kwa asilimia nne yenye thamani kubwa ya asilimia 61.5.

"Kuliko makandarasi wazawa ambao ni wengi kwa idadi ya asilimia 94.6 ambapo wanatekeleza miradi mingi asilimia 96 yenye thamani ndogo ya asilimia 38.5 tu," alisema.

Kadhalika, ni wazi kuwa, uwiano huo usio wa usawa katika utekelezaji wa miradi kati ya wazawa na wageni, ni changamoto ambayo inahitaji ufumbuzi wa haraka.

"Sababu ya kwanini hali iko hivi zinajulikana ikiwamo makandarasi wa ndani hawana uwezo wa kifedha, kimitambo na kitaalam, kuweza kushindana kwenye zabuni za kazi na makandarasi wa nje. Hivyo, kazi zote kubwa za ujenzi wa barabara zikitangazwa, kampuni za nje hushinda hasa ya nchini China," alisisita Bashungwa.

Alisema vipaumbele na maagizo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika sekta hiyo ni kuona ushiriki mkubwa zaidi wa makandarasi wazawa katika kazi za ujenzi wa miradi (Local Content).

Vile vile, alisema ili kutekeleza vipaumbele na maagizo hayo, serikali imekuja na mikakati mbalimbali ya kuwalinda wazawa ikiwamo, Sheria ya Ununuzi wa Umma imefanyiwa marekebisho.

"Kwa kuongeza kiwango cha thamani ya mradi ambao utatekelezwa na makandarasi wa ndani tu, bila kushindanishwa na makandarasi wa nje," alisema.

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Daniel Chongolo, aliiagiza serikali kufanyia kazi kero zote zinazowakabili makandarasi wazawa.

"Kero kubwa kwa makandarasi wazawa hata hapa nikiwa na karatasi niwaambie waandike kero zao kubwa itakuwa ni malipo lazima Wizara ya Fedha kuhakikisha kuwa malipo ya makandarasi wazawa hayachelewi kama ilivyo sasa kwani hali hii ni sababu ya kuwarudisha nyuma," alisema Chongolo.

## Anayedaiwa kuua mtoto kwenda kuishi Dar kupimwa afya ya akili

**Na Francis Godwin,** IRINGA

JESHI la Polisi mkoani Iringa, limeanza kumchunguza afya ya akili Johari Mbuma (19) mkazi wa Mawelewele, Manispaa ya Iringa, anayetuhumiwa kumuua mtoto wake wa kike mwenye umri wa miezi tisa ili aende kuishi Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, Kamishna Msaidizi (ACP) Allan Bukumbi, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa kutokana na binti huyo kumuua mtoto wake kwa kumtumbukiza kwenye ndoo ya maji, uchunguzi zaidi unaendelea ikiwa ni pamoja na kumpeleka kwa daktari ili kupimwa afya ya akili.

"Tayari tumekamilisha kumhoji mtuhumiwa na tunatarajia kumpeleka kwa daktari kwa ajili ya vipimo vya afya ya akili ambao ni utaratibu wa kawaida kwa watuhumiwa wote wa mauaji, alisema Bukumbi na kubainisha kwamba baada ya uchunguzi, atafikishwa mahakamani.

Akizungumza juzi wakati akihojiwa na uongozi wa serikali ya mtaa wa Mawelewela, Mbuma alisema maisha ambayo amekuwa akiishi Iringa yalikuwa magumu na baada ya kuwasiliana na mama yake, alimtaka aende kuishi Dar es Salaam lakini masharti ni kwamba aende bila mtoto.

"Mama alisema kwa kuwa nimekatisha masomo kutokana na ujauzito na nataka kwenda kuishi naye Dar es Salaam, basi niende mwenyewe bila mtoto na kama nitakwenda na mtoto nisifikie nyumbani kwake. Kutokana na shrti hilo ndiyo maana nikalazimika kumnyonga mtoto wangu na kumtupa kwenye ndoo ya maji ili nisafiri kwenda kuishi na mama Dar es Salaam," alisema.

Kabla ya kupata wazo la kuua mtoto, alisema alifunga safari hadi eneo la Zizi la Ng'ombe kwa rafiki yake na iwapo angemkuta, angemtelekeza mtoto huyo kwa rafiki yake na yeye kusafiri kwenda Dar es Salaam. Lakini baada ya kumkosa, aliamua kumnyonga shingo na kumtupa kwenye ndoo ya maji iliyokuwa ndani ya choo cha rafiki yake huyo kisha kutoweka.

Alisema mwanamume ambae alimpa ujauzito, yuko Pawaga wilaya ya Iringa na kuwa tangu ampe ujauzito, hajawahi kuwasiliana tena wala hakuna huduma yoyote aliyokuwa akiituma kwa ajili ya kumsaidia mahitaji.

Kutokana na hali hiyo, alimpigia mama yake na kumwomba msamaha kwa kukatisha masomo ya sekondari.

Mbuma alikuwa miongoni mwa wanafunzi wa kidato cha nne wanaotarajia kuhitimu masomo mwaka huu.

Alisema anajutia uamuzi huo aliochukua lakini hakuwa na namna ya kufanya zaidi ya kufanya hivyo ili aende kuanza maisha mapya Dar es Salaam .

Katika hatua nyingine Jeshi la Polisi Mkoa wa Iringa, limemkamata Edger Mbalazi ambaye alikuwa ametoroka mahakamani baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka 20 jela kwa kosa la kupatikana na meno ya tembo.

Kamanda Bukumbi alisema Mbalazi atafikishwa mahakamani kwa ajili ya tuhuma zinazomkabili huku akiendelea kutumikia kifungo chake cha awali cha miaka 20 jela ambacho tayari kilitolewa na mahakama.


Lindi Jumbo Limited

# VACANCIES

**About Lindi Jumbo Ltd**

Lindi Jumbo is a Tanzanian graphite mining company developing a high-grade, low-cost mine expected to begin production in early 2024. The company is well-positioned to capitalize on the growing demand for graphite as the world transitions to a clean energy economy. Lindi Jumbo is committed to sustainable mining practices and contributing to the social and economic development of the Lindi Region.

**Process Discipline**
- Process Controller
- Plant Operators
- Equipment Operators (Forklift & Front-End Loaders)

**Engineering Discipline**
- Maintenance Planner
- Millwrights/Electricians
- Fitters
- Boilermakers
- Instrumentation Tech
- Instrumentation Mech

**Administration Discipline**
- GP/Occupational Health
- Occupational Health Nurse
- ESG Officer

➢ **Location: Matambarale, Ruangwa District, Tanzania.**

➢ **Closing Date: 30 November 2023, 4:00PM (GMT+2)**

SCAN ME

To apply or view more details visit: https://jobportunities.net/jobs_search.aspx or scan the QR Code.

*For assistance on the portal, please contact Lindi Jumbo at +255 22 260 2770.*

*Alternatively send an email via the recruitment portal's Contact Us page.*

177231

# Hakimu amhoji baba kuruhusu bintiye kushika dawa kulevya

Na Grace Gurisha

HAKIMU Mkazi Mkuu Romuli Mbuya wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, amemhoji baba mzazi wa Asina Ally anayetuhumiwa kusafirisha dawa za kulevya, sababu za kumpa rukhsa binti yake kushika dawa za kulevya.

Asina ambaye ni Mkazi wa Magomeni Mapipa, anatuhumiwa kukutwa akisafirisha dawa za kulevya aina ya mirungi zenye uzito gramu 856.9 kinyume cha Sheria ya Kudhibiti Dawa za Kulevya.

Mzee Mahmood alijikuta katika wakati mgumu jana baada ya mtoto wake Asina kumaliza kusomewa shtaka lake la kusafirisha dawa za kulevya na yeye kutaka kumdhamini. Alijikuta akiulizwa maswali na Hakimu Mbuya.

Kabla ya maswali hayo, Hakimu Mbuya alitoa masharti ya dhamana kwamba mshtakiwa ili adhaminiwe, anatakiwa awe na Sh. milioni tano na pia awe na mashahidi wawili wenye barua za utambulisho, kila mmoja atatia saini bondi ya kiasi hicho cha fedha.

**Hakimu:** Nikiwaangalia tu ninaona ni mtu na baba yake.

**Mzee:** Ni kweli.

**Hakimu:** Kwanini unamruhusu mtoto wa kike kushika dawa za kulevya?

**Mzee:** Mimi nilikuwa zangu Uganda, ninarudi nyumbani ndipo ninakutana na haya, si unajua damu nzito, ndiyo maana nipo hapa.

**Hakimu:** Ulimpeleka madrasa kweli?

**Mzee:** Nilimpeleka.

**Hakimu:** Ulimfuatilia kama anaswali?

**Mzee:** Anaswali sala tano.

**Hakimu:** Sala tano na dawa kweli? Hebu waangalieni watoto na mhakikishe kama kweli wanaswali. Mzee si umeyaona haya?

**Mzee:** Nimeyaona.

**Hakimu:** Haya mzee, niambie kazi yako inayokuingizia kipato.

**Mzee:** Kutokana na hali yangu ya kiafya kwa sasa nimepumzika nyumbani, ninasubiria watoto waniletee riziki.

**Hakimu:** Unaona sasa, ndiyo haya sasa hawa wanaingia kwenye dawa za kulevya.

**Mzee:** Hapana si moja kwa moja kwamba ninawategemea wao, nina nyumba ya urithi inaniingizia kodi, kwa sababu kwa sasa kazi yangu ni kula na kwenda msikitini.

**Hakimu:** Umesikia maelezo ya wadhamini?

Baada ya maswali hayo na mengine, mshtakiwa Asina aliachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza masharti yaliyowekwa na mahakama.

Awali Wakili wa Serikali, Cathbert Mbilingi alidai kuwa Asina anatuhumiwa kutenda kosa hilo Julai 14 mwaka huu akiwa eneo la Tandale, Magomeni Mapipa, ndani ya Wilaya ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam. Alikutwa na mirungi yenye uzito wa gramu 856.9.

Mshtakiwa huyo alikana kuhusika na tuhuma hizo. Wakili Mbilingi alidai kuwa upelelezi umekamilika na kuomba tarehe nyingine ili amsomee mshtakiwa maelezo ya awali. Hakimu Mbuya aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba 7, mwaka huu.

Hata hivyo, baada ya mshtakiwa kusomewa mashtaka yake, hakimu alitaka kujua kazi anayojishughulisha. Asina alidai anauza nguo za kike, lakini hana leseni ya biashara. Anawauzia watu mikononi mithili ya machinga.




Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Saada Mkuya (katikati waliosimama), akishuhudia wakati Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kushoto -waliokaa) na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Yusuph Mwenda wakitia saini, mjini Zanzibar jana, makubaliano yatakayotoa fursa kwa benki hiyo kutumika kukusanya malipo mbalimbali ya SMZ kupitia mtandao na mfumo wa kidijitali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

## Kesi unyang'anyi milioni 78/- kunguruma Desemba 7

Na Kulwa Mzee

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu Desemba 7, mwaka huu inatarajia kuanza kusikiliza ushahidi wa kesi ya unyang'anyi wa kutumia nguvu na kujipatia Sh. milioni 78.6 inayowakabili watu watatu akiwamo askari namba F 5867 Koplo Khamisi.

Shauri hilo lilikuja jana mahakamani kwa ajili ya kusikilizwa, lakini lilikwama kwa sababu Wakili wa Serikali, Judith Kyamba anayeiwakilisha Jamhuri alikuwa na changamoto za kiafya.

Wakili Judith aliitaarifu mahakama mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Amir Msumi kuwa hawezi kuendesha kesi hiyo kwa kuwa hakuwa vizuri kiafya. Shahidi pia hakuwa vizuri kiafya.

Upande wa Jamhuri uliomba kuahirisha shauri hilo hadi tarehe nyingine na mahakama iliridhia shauri hilo lianze kusikilizwa Desemba 7 mwaka huu.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Sia Tarimo na Nassoro Athumani. Katika hati ya mashtaka, inadaiwa kuwa Mei Mosi 2022, katika eneo la Ukonga Airport, Karakata, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, washtakiwa waliiba Sh. 78,600,000, mali ya Zawia Shabani.

Inadaiwa kuwa kabla na baada ya kuchukua fedha hizo, walitishia kutumia nguvu kuchukua kiasi hicho cha fedha.

**Wakili Judith aliitaarifu mahakama mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Amir Msumi kuwa hawezi kuendesha kesi hiyo kwa kuwa hakuwa vizuri kiafya. Shahidi pia hakuwa vizuri kiafya.**

# Wakufunzi wafundwa mtanziko wa kimaadili

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Oslo nchini Norway, kimeanza kutoa mafunzo ya maadili ya kitabibu kwa watoa huduma za afya na wakufunzi wa kozi mbalimbali katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya.

Mafunzo hayo yanalenga watumishi hao kuwasaidia kukabiliana na mtanziko wa kimaadili wanapotoa huduma kwa wananchi.

Mafunzo hayo ya siku nne yanayotolewa kupitia mradi wa ETHIMED unaofadhiliwa na serikali ya Norway yanalenga kuwajengea uwezo watoa huduma za afya nchini, kutatua vikwazo vya mtanziko wa kimaadili wanavyokutana navyo wakati wa utoaji huduma kwa wagonjwa.

Mratibu wa programu ya Ethimed Tanzania, Lucas Kitula, aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku nne.

Alisema programu hiyo ya miaka mitano inajumuisha utafiti kutoa mafunzo na kuanzisha kamati ya maadili ya kitabibu Tanzania itakayojikita kutatua vikwazo vya maadili ya kitabibu tofauti na kamati ya kinidhamu ambayo imekuwepo kwa ajili ya kuwajibisha wanaokiuka masuala ya kinidhamu.

Kitula alisema Tanzania itakuwa nchi ya kwanza kwa ukanda wa Afrika Mashariki kuanzisha Kamati ya Maadili ya kitabibu hospitalini baada ya nchi nyingine, ikiwemo Norway kuwa na kamati hizo kwenye hospitali zao zote.

"Hatuzungumzii maadili ya kinidhamu ambayo kuna kamati zake huwa zinafanya kazi ya kuwajibisha, lakini sisi tunaangalia ule mtanziko anaokutana nao mtoa huduma za afya kwa mgonjwa, mfano mgonjwa anakataa matibabu kutokana na imani yake je mtoa huduma atafanyaje," alisema Kitula.

Mhadhiri Msaidizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mtafiti wa Maadili ya Kitabibu, Shija Kahumba, alisema walibaini watoa huduma za afya wanakutana na mitanziko kwenye kufanya maamuzi sehemu zao za kutoa huduma kwa wagonjwa hali inayosababisha kupata msongo wa mawazo.

Kahumba alisema licha ya kuwepo kwa kamati za nidhamu kwa watoa huduma za afya, lakini kamati hiyo haitakua kamati za maadili za kuadhibu bali itajikita kwenye utoaji wa miongozo ya kiuweledi itakayosaidia kutatua mtanziko wa kimaadili kwa kujadiliana pamoja na wagonjwa ili kuzuia matatizo.

Alisema kamati hiyo itahusisha watu tofauti wakiwemo wanasheria,viongozi wa dini, ambao watapatiwa mafunzo maalumu baada ya kuundwa kwa kamati hiyo, Februari 2024 na kwamba mafunzo yatakuwa endelevu kwenye hospitali zote kubwa, ili kupata wakufunzi watakaoishusha elimu hiyo ngazi ya hospitali za wilaya na vituo vya afya.

Mkufunzi wa maadili ya kitabibu na mwezeshaji wa mafunzo wa Chuo cha Oslo, Norway, Prof. Bert Molewijk, alisema Tanzania itakuwa miongoni mwa wanufaika wakuu wa programu hiyo ya mafunzo yatakayosaidia kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini.

Aliongeza kuwa kamati za maadili ya kitabibu zitawasaidia watoa huduma za afya kujadili mbinu bora za namna ya kuwahudumia wagonjwa pale wanapokua na mtanziko wa kimaadili, ili kufanya maamuzi sahihi yatakayoleta matokeo chanya kwenye suala la matibabu.

# Ziara ya Rais Samia India yaendelea kuleta neema

**Na Romana Mallya**

ZIARA ya Rais Samia Suluhu Hassan India imeendelea kuzaa matunda baada ya ujumbe wa wafanyabiashara unaojumuisha kampuni 30 kutoka India kukutana na jumuiya ya wafanyabiashara wa Tanzania kujadili namna ya kukuza biashara na ushirikiano.

Ujumbe huo wa wafanyabiashara hao ukiongozwa na Waziri wa Nchi anayeshughulikia Mambo ya Nje na Bunge wa India, Shri Muraleedharan, upo nchini kwa siku tatu. Jana walikutana na wafanyabiashara wazawa katika Ubalozi wa India nchini.

Katika mkutano huo, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, alisema ujio huo ni ushuhuda wa wazi kuwa ziara ya Rais Samia India ina matunda mengi.

Alisema nchi hizo zina ushirikiano mzuri wa kiuchumi katika maeneo ya biashara na uwekezaji.

Waziri Muraleedharan alisema miaka ya hivi karibuni wameshuhudia ziara za kibiashara kati ya nchi hizo zinazochangia kubadilishana mawazo na namna nzuri ya kufanya biashara.

"Kwa uwekezaji wa India Tanzania umeongezeka hadi Dola bilioni 3.7 ukihusisha sekta mbalimbali zikiwamo elimu, famasia, elimu madini na uchakaji bidhaa za kilimo," alisema.

Waziri Muraleedharan alisema ujenzi wa eneo maalum la viwanda lenye ukubwa wa ekari 1,000 linalotarajia kujengwa Tanzania, utachangia uwekezaji kutoka India kuja kuwekeza Tanzania.

Rais na Mwenyekiti wa Bodi ya Chemba ya Biashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) Vicent Minja, alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, mataifa hayo yameshuhudia ongezeko kubwa la biashara kutoka Dola bilioni 2.6 mwaka 2017/18 hadi Dola bilioni 6.5 mwaka 2022/23.

Alisema India imekuwa mshirika wa nne wa kibiashara wa Tanzania, ikiwa na jumla ya miradi 631 ya uwekezaji inayofikia Dola bilioni 3.7.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Biashara Tanzania (TANTRADE), Latifa Khamis, alisema katika kukuza biashara kati ya nchi hizo, TANTRADE iliandaa, kuratibu na kushiriki mikutano mbalimbali ya kibiashara na maonyesho ya biashara nchini na India.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Raphael Maganga, alisema majadiliano hayo yanapaswa kuwa jukwaa la kuunda ushirikiano muhimu ambao utafaidisha nchi hizo, hivyo wanatarajia kuona ushirikiano zaidi katika miaka michache ijayo.

Balozi Pradhan Binaya alimshukuru Mwenyekiti wa Jukwaa la Biashara kati ya Tanzania na India, Gagan Gupta kwa kuandaa mkutano huo.

Mkuu wa International Fortis Health Care Limited na kiongozi wa msafara wa Shirikisho la Viwanda India (CII), Renu Vij, alisema ujumbe huo umelenga kuwasiliana na wanaowakilisha sekta za miundombinu, elimu, huduma za afya, kilimo madini, nishati na dawa.




Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Hassan Abbas (kulia), akikabidhi moja kati ya mizinga ya nyuki iliyotolewa na Benki ya NMB kwa Mwakilishi wa Kikundi cha Juhudi Msingisi, Naomi Mbuhe, wakati wa uzinduzi wa kitaifa wa programu ya ugawaji mizinga hiyo, kwa wafugaji wa mikoa ya Morogoro, Tabora na Njombe, uliofanyika katika Msitu wa Msingisi, Kijiji cha Msingisi, wilayani Gairo, mkoani Morogoro jana. Wa pili kulia ni Ofisa Mkuu wa Biashara za Serikali wa Benki hiyo, Alfred Shao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Upelelezi wakwamisha kesi ya Mkurugenzi wa Temeke

**Na Kulwa Mzee**

UPANDE wa Jamhuri umedai upelelezi wa kesi inayomkabili aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Lusubilo Mwakabibi na Mratibu wa Mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam (DMDP) Edward Haule haujakamilika.

Wakili wa Serikali Monica Ndakidemi alidai hayo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Evodia Kyaruzi.

Wakili Ndakidemi alidai upelelezi wa shauri hilo haujakamilika, hivyo aliomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa.

Mshtakiwa Mwakabibi jana hakufika mahakamani. Mdhamini wake alidai mteja wake alikuwa Mbeya kwenye msiba wa mdogo wake.

Upande wa Jamhuri uliomba shauri hilo lipangiwe tarehe nyingine ya kutajwa. Mahakama ilipanga Desemba 21 mwaka huu.

Mwakabibi na Haule wanakabiliwa na mashtaka mawili ya matumizi mabaya ya madaraka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Kwa mara ya kwanza, washtakiwa hao walifikishwa mahakamani huko Agosti 20, 2021 wakikabiliwa na mashtaka mawili ya matumizi mabaya ya ofisi na madaraka.

Katika shtaka la kwanza la matumizi mabaya ya ofisi, washtakiwa wanadaiwa kutenda kosa hilo, kati ya Machi 2020 na Machi 2021 katika Manispaa ya Temeke.

Inadaiwa kuwa Mwakabibi, akiwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, na Haule akiwa Mratibu wa Mradi wa DMDP na wakiwa waajiriwa wa manispaa hiyo, walielekeza ujenzi wa stendi ya mabasi eneo la Buza, kiwanja ambacho kinamilikiwa na Dayosisi ya Kanisa la Anglikana bila kuwa na rukhsa.

Katika shtaka la pili la matumizi mabaya ya madaraka, wanadaiwa kutenda kosa kati ya Machi 2020 na Machi 2021 katika eneo hilo. Inadaiwa kuwa washtakiwa kwa makusudi walitumia madaraka yao vibaya na kinyume cha kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Ardhi na Kifungu cha 3,4,5,7 na 11 cha Sheria ya Ardhi ya Mwaka 2019.

# Biteko aagiza kuandaliwa mpango upatikanaji gesi

**Na Teresia Mhagama**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ameagiza Bodi na Menejimenti ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuja na mpango wa muda mrefu utakaoonesha jinsi nchi itakavyoongeza gesi asilia ili muda wote kuwe na hazina ya gesi.

Nishati hiyo inatumika kuzalisha umeme, viwandani, majumbani na magari.

Dk. Biteko aliagiza hayo jana wakati wa kikao chake na Bodi na Menejimenti ya TPDC ambacho kililenga kufahamiana, kubadilishana mawazo juu ya utendaji kazi huku akielekeza matarajio ambayo nchi inayahitaji toka TPDC.

"TPDC tujiulize uwezo wetu wa kuzalisha gesi asilia unaweza kujibu mahitaji yetu ya gesi? Tujiulize hili na tuchukue hatua. Tutambue kuwa mahitaji ya gesi asilia ni makubwa kwa sasa kwani dunia inahama kutoka matumizi ya mafuta na kwenda kwenye gesi asilia, hivyo lazima tujipange.

"Pia tukumbuke tumetia saini makubaliano ya kusafirisha nishati hii kwenda Uganda, Zambia na Kenya, hivyo lazima tuwe na gesi ya kutosha," alisema Dk. Biteko.

Vilevile, kiongozi huyo aliitaka TPDC kutokuwa na urasimu katika uchukuaji wa uamuzi mbalimbali ikiwamo kwenye shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia ili kutorudisha nyuma sekta hiyo nchini.

Kuhusu maelekezo aliyoyatoa wakati wa ziara yake katika Kisiwa cha Songosongo mkoani Lindi na Kijiji cha Madimba na Msimbati mkoani Mtwara, Dk. Biteko alisisitiza kuwa maisha ya wananchi katika maeneo hayo ambako kuna visima na mitambo ya gesi asilia, lazima yabadilike na wapewe huduma bora ikiwamo maji, umeme, matibabu na usafiri.

"Ninashukuru mmeanza kufanyia kazi kwa haraka maagizo niliyoyatoa ikiwamo kuweka taa za barabarani Kijiji cha Msimbati, kupeleka umeme wa uhakika Madimba na Msimbati unaotoka kwenye mitambo ya gesi asilia, kupeleka kivuko kisiwa cha Songosongo na malipo ya mafao kwa

wastaafu wa Knight Support ambao walikuwa wakilinda mitambo na visima vya gesi asilia Songosongo ambao hawakulipwa muda mrefu, watu hawa wanahitaji huduma bora," alisema Dk. Biteko.

Naibu Waziri Mkuu pia aliiagiza TPDC kupita kwenye halmashauri zote nchini zinazopokea ushuru wa huduma kutokana na shughuli za mafuta na gesi asilia kufanyika kwenye halmashauri hizo ili ijihakikishie kwamba fedha hizo zinakwenda pia kwenye vijiji/maeneo ambayo shughuli za uzalishaji wa gesi asilia zinafanyika.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Mussa Makame alimweleza Naibu Waziri Mkuu kuwa shirika linaandaa Mpango Mkakati (Corporate Strategic Plan) ambao utaweka mikakati ya shirika kwa kipindi cha miaka 10 na zaidi ili kuwezesha upatikanaji gesi asilia ya kutosha kwa matumizi ya ndani na kuwekeza zaidi katika mnyororo wa thamani wa mafuta na gesi.

Lengo la mpango huo ni kukuza matumizi ya gesi asilia na hivyo kuchochea biashara katika Ukanda wa Afrika Mashariki.

Pia alieleza mipango ya utekelezaji mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Uganda kuja Tanzania na Mradi wa Gesi ya Kusindika (LNG) ambao majadiliano yamekamilika na mikataba iko kwenye hatua za kuidhinishwa.

Vilevile, kiongozi huyo wa TPDC alisema utafutaji mafuta na gesi asilia katika Kisiwa cha Songosongo Magharibi unatarajiwa kuanza Septemba 2025 pamoja na utafutaji mafuta kitalu cha Eyasi Wembere.

Mwenyekiti wa Bodi ya TPDC, Balozi Ombeni Sefue

alimshukuru Naibu Waziri Mkuu kwa maelekezo yake ambayo yamewapa hamasa ya kufanya kazi na kumwahidi watatoa ushirikiano kwake ili kuinua zaidi sekta ya mafuta na gesi asilia nchini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Madereva bodaboda, bajaji kero barabarani

**SEKTA** binafsi katika usafirishaji imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la ajira kwa vijana nchini kutokana na vijana wengi kupata shughuli ya kujipatia kipato.

Usafiri wa umma mwanzo ulikuwa ukitegemewa kutolewa na serikali kwa mabasi maarufu kwa upande wa Dar es Salaam yalijojulikana kama UDA.

Baadaye yakaja magari ya watu binafsi ambayo yalipewa jina la daladala kutokana na wakati huo kutoza nauli ya Shilingi tano na kupata umaarufu wa jina hilo.

Lakini, kutokana na dunia sasa kuwa kama kijiji, mambo mengi yamebadilika ikiwamo ya usafiri kutokana na kuiga kutoka nchi nyingine.

Majirani zetu Uganda walianza kutoa huduma ya usafiri wa umma kwa kutumia pikipiki na kuuita usafiri huo bodaboda kutokana na uharaka wake wa kukutoa sehemu moja hadi nyingine.

Tanzania ukaingia usafiri huo kwa kasi ya ajabu na pengine hata kuwashinda waanzilishi. Uganda walikuwa wakipakia abiria wawili kwenye pikipiki moja, lakini huku kwetu wanapakia mpaka abiria wanne pamoja na dereva ni idadi ya watu watano na kuupa jina la 'mshikaki'.

Vivyo hivyo kwa usafiri wa bajaji ambao awali ulikuwa ni kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa miguu, lakini sasa umekuwa usafiri wa umma ambao umeigwa kutoka nchini India.

Kuongezeka kwa usafiri huu wa bodaboda na bajaji kumesaidia kupunguza vijana wanaokaa vijiweni kwa kukosa ajira na sasa wanafanyakazi ya kusafirisha abiria.

Hata hivyo, madereva wengi wa vyombo hivyo wamekuwa kero kubwa barabarani kwa kutofuata sheria za barabarani. Wengi wa madereva hao ndio chanzo cha ajali kwa kupita katikati ya magari na kuyakwaruza au kusababisha uharibifu na pia kuwagonga watembea kwa miguu.

Madereva wa vyombo hivyo wameachwa wakifanya uvunjifu huo wa sheria za barabarani mpaka wanajiona kuwa ni haki yao kuvunja sheria.

Kwenye taa nyekundu wanapita, wanakatiza mbele ya magari mengine bila tahadhari na wanapoyagonga magari ni rahisi kukimbia kwa sababu wana uwezo wa kukatisha popote bila kukamatwa.

Serikali imesema inafanya mchakato wa kuharakisha kuingia katika mfumo unaotumika kutoa faini moja kwa moja kwa madereva wanaochezea mfumo wa ufuatiliaji wa magari (VTS) na kukiuka sheria za barabarani ikiwamo kuendesha kwa mwendokasi.


Mfumo huo unaelezwa kuwa ni mzuri sana kwa sababu ni tofauti wa kusubiri mpaka trafiki apige tochi, huu ukifanya kosa tu au ukiendesha mwendokasi unakupiga faini moja kwa moja.

Tunaomba mfumo huu usiangalie tu madereva wa magari, uangalie pia madereva wa bodaboda na bajaji ili sheria iwaguse pia.

LATRA ina jukumu la kutathmini mchakato wa mitihani wa kuwatambua na kuwasajili madereva wanaofanya mitihani ya madereva na kufaulu.

Mfumo huo kama utaruhusiwa kudhibiti magari yote yanayotumia barabara ikiwamo ya watu binafsi na ya serikali, mwenendo wa madereva na tabia zao barabarani utafuatiliwa na kupunguza kiwango kikubwa cha ajali za barabarani na vifo vya watu ambao hawana hatia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# NEC ikumbuke mawasiliano

**TUME** ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imeanza kufanya maandalizi mbalimbali ya uchaguzi wa 2025, ikiwamo kufanya jaribio la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kwenye baadhi ya maeneo.

Wakati ikiwa katika mchakato huo, zimeanza kujitokeza changamoto kwenye baadhi ya sehemu kama ukosefu wa mawasiliano ya simu yanayoweza kusababisha mchakato huo kuwa mgumu.

Katika zoezi hilo, NEC itatumia mashine za Biometric Voters Registration (BVR) zenye vifaa mbalimbali vinavyowasiliana ili kuchukua na kutunza taarifa za wapigakura wa mikoa ya Tabora na Mara.

BVR kits hizo ni mpya tofauti na zile zilizotumiwa kwenye kuboresha daftari la kudumu la wapigakura mwaka 2015 na 2019 zenye vifaa mbalimbali vinavyowasiliana ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za kila mpigakura.

Lengo la kufanya zoezi hilo kuwa ni kupima uwezo wa vifaa na mifumo ya uandikishaji itakayotumika wakati wa uboreshaji wa daftari la hilo unaotarajiwa kufanyika nchi nzima pale NEC itakapopanga ratiba.

Hata hivyo, wakati huu ambao tume imechagua maeneo hayo machache ya kufanyia majaribio ya kuboresha daftari hilo, inaonekana kuwa katika wilaya ya Rorya baadhi ya maeneo yake hayana mawasiliano ya simu.

Wakazi wa Wilaya ya Rorya mkoani Mara wanasikika wakisema hayo juzi, viongozi wa NEC walipofika kwa ajili ya kuboresha daftari, na kwamba mawasiliano ya simu za mkononi ni tatizo.

Kwa kuwa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa tume hiyo, Ramadhani Kailima, ni kwamba itatumia BVR kits zenye vifaa vinavyowasiliana ili kuchukua na kutunza taarifa za wapigakura, ni vyema tatizo la Rorya likatafutiwa ufumbuzi haraka.

Ninadhani katika mazingira hayo yanayolalamikiwa na wakazi wa Rorya, inawezekana kukawa na ugumu, hivyo kama inawezekana, kampuni za simu za mkononi zingefanya mchakato wa kuweka mawasiliano kabla ya kuanza uboreshaji wa daftari hilo kwa nchi nzima.

Wananchi wamefikisha malalamiko kwa NEC, hivyo ninadhani haina budi kuwasiliana na kampuni za simu ili kuangalia iwezekanavyo wa kuweka mawasiliano haraka, iwe rahisi kwa wananchi wa huko kuchukuliwa kumbukumbu zao na kuingizwa katika daftari hilo.

Kama tume inatumia BVR zenye vifaa vinavyowasiliana ili kuchukua na kutunza taarifa za wapigakura, wakati maeneo mengine ya nchi hakuna mawasiliano, nidhani hilo linatakiwa kufanyiwa kazi haraka.

Aidha, NEC, inaboresha daftari kwa kushirikisha vyama vya siasa kwa kuweka wakala mmoja katika kila kituo cha kuandikisha wapigakura ili kushuhudia na kujiridhisha kuhusu taratibu zitakazotumika wakati wa uboreshaji wa majaribio wa daftari.

Utaratibu huo wa uboreshaji wa taarifa kwa njia ya mtandao hautawahusisha wapigakura wapya wanaotaka kuandikishwa kwa mara ya kwanza na waliopoteza kadi zao au kuharibika.

Hatua hiyo ya NEC inalenga kuwezesha wapigakura ambao wameandikishwa na wapo kwenye daftari hilo, kuanza mchakato wa kubadili na kuboresha taarifa zao na kituo cha kupigia kura.

Kwa maana hiyo, iwapo mpigakura amehamia wilaya au mkoa mwingine, taarifa zake zitarekebishwa kwa kutumia mawasiliano ya simu ya mkononi, ili kuweka mambo sawa.

Ni wazi kwamba, tangu uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, wapo baadhi ya Watanzania ambao huenda wamepoteza kadi zao au kuhama maeneo ya awali, hivyo ni muhimu mchakato ufanyike ili wapewe vitambulisho vipya au wabadilishiwe maeneo kutoka ya awali kuwa ya sasa.

Vinginevyo wanaweza kujikuta wakipoteza haki yao ya kuchagua viongozi wanaowataka. Kwa kawaida majina huwa yanabandikwa kwenye vituo vya kupigia kura ili wale wote waliojiandikisha wahakiki na kujiandaa na kupiga kura.

Wakati tume inafanya majaribio kwa mikoa miwili kabla ya kuzunguka nchi nzima, ninadhani ingeelekeza nguvu katika kutatua tatizo la ukosefu wa mawasiliano ambayo wananchi wa Rorya wamelalamikia.

Yawezekana tatizo kama likawapo pia maeneo mengine ya nchi, hivyo si vibaya kuanza kufuatilia changamoto hiyo kwa upana wake ili wakati wa uboreshaji wa daftari kwa nchi nzima iwe imetatuliwa.

HABARI KITAIFA

# Mwanafunzi aliyekwenda kufanya kazi za ndani arejeshwa shuleni

**Na Moses Ng'wat,** ILEJE

MKUU wa Wilaya ya Ileje, Farida Mgomi kwa kushirikiana na wazazi, wamefanikiwa kumrejesha shuleni mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Ileje aliyekatisha masomo na kwenda kufanya kazi za ndani katika Mji wa Tunduma.

Inaelezwa kuwa mwanafunzi huyo (jina tunalo) alilazimika kukatisha masomo yake baada ya wazazi wake kudaiwa kushindwa kumudu kuchangia gharama za chakula shuleni huko.

Hatua ya kumrejesha shuleni mwanafunzi huyo imechukuliwa siku chache baada ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Francis Michael kumwagiza Mkuu wa Wilaya hiyo kuhakikisha anamrejeaha shuleni mwanafunzi huyo wa kidato cha kwanza ili aendelee na masomo.

Mbali na mwanafunzi huyo, Mkuu wa Mkoa pia aliagiza kurejeshwa shuleni wanafunzi wengine watatu ambao wazazi wao waliwahamisha na kuwapeleka katika shule za kutwa kwa kisingizio cha kukosa michango ya chakula.

Akimkabidhi mwanafunzi huyo kwa uongozi wa shule mbele ya Mkuu wa Mkoa juzi, Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Farida, alisema jitihada za kumrejesha shuleni mwanafunzi huyo zimetokana na wazazi kukubali na kutoa ushirikiano kwake.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, kurejea kwa mwanafunzi huyu ni faraja kwa uongozi wa wilaya kwani ni adhima ya serikali kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anapata haki ya msingi ya kusoma. Lengo la kuanzishwa shule ya wasichana wilaya ya Ileje ni kuwakomboa watoto wa kike," alisema.

Kuhusu wanafunzi wengine waliondolewa shuleni huko na wazazi wao, Farida alisema jitihada za wanafunzi wawili kurejeshwa shuleni zinaendelea, huku akifafanua kuwa mwanafunzi wa tatu alihamishiwa mkoani Morogoro ambako anaendelea vizuri na masomo baada ya kuchukuliwa na baba yake mdogo.

Mkuu wa Mkoa baada ya kushuhudia kurejeshwa shuleni mwanafunzi huyo, alitoa maelekezo mahususi kwa Ofisa Elimu wa Mkoa huo, Michael Lugola, kuhusu wanafunzi wa kike katika Mkoa wa Songwe, akimtaka kuhakikisha anatembelea shule zote za bweni za wasichana ili kubaini wanafunzi walioacha shule kwa kukosa fedha za chakula ili wawarejeshe kama ilivyofanyika katika Shule ya Wasichana Ileje.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkuu wa shule hiyo, Sharon Kadinde, shule hiyo iliyoanzishwa mwaka huu, ilipangiwa wanafunzi 75, lakini walioripoti ni 71.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari (katikati), akiwasilisha mada kwa wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar walipotembelea Ofisi za Makao Makuu ya Mamlaka hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. Kamati hiyo, inaongozwa na Mwenyekiti wake, Yahya Rashid Abdulla. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zitto: Wizara iondoe maofisa wa TFS Kasulu

**Na Julieth Mkireri,** KASULU

CHAMA cha ACT Wazalendo kimemtaka Waziri wa Maliasili na Utalii kuondoa maofisa wa Wakala wa Huduma ya Misitu (TFS) wilayani Kasulu kutokana na kulalamikiwa kupoka ardhi ya wananchi.

Vilevile, kimemtaka waziri huyo kuzungumza na wananchi wa Kata ya Kagera Nkanda wilayani humo kwa lengo la kupata majawabu ya kero zinazowakabili.

Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe alitoa kauli hiyo juzi katika mkutano wa hadhara baada ya wananchi kulalamika kuwa maofisa wa taasisi hiyo kwa kushirikiana na viongozi wa Wilaya ya Kasulu wanapoka maeneo yao ya ardhi kwa madai ni sehemu ya hifadhi na kisha kuwakodishia kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Zitto alisema maofisa hao wamekosa uhalali wa kuendelea kuwahudumia wakazi wa Kasulu kwa kuwa wamelenga kujinufaisha binafsi badala ya kusimamia miiko ya kazi zao.

"Kama ardhi imechukuliwa kwa matumizi ya hifadhi, ibaki hivyo. Hiki kitendo cha kuwataka wananchi walipie fedha ili kutumia ardhi hiyo ni ufisadi mkubwa.

"Mbaya zaidi, fedha hizi zinaingia kwenye mifuko ya watu binafsi bila ya kutolewa risiti yoyote," Zitto alidai.

Akizungumzia changamoto ya mipaka kati ya Pori la Akiba la Kagera Nkanda na Msitu wa Makere Kusini, Zitto alisema mipaka ya mwaka 1956 ilitenganisha eneo la hifadhi na mipaka ya kijiji, lakini sasa hifadhi imeingia katika maeneo ya kijiji.

Alisema ni jambo la kusikitisha kuona eneo la hifadhi linaongezeka kwa kuchukua maeneo ya wanakijiji ilhali kila siku watu wanaongezeka.

Kiongozi huyo alisema kilichotakiwa kufanyika ni kuongeza eneo la kijiji kwa kuwa idadi ya watu iliyokuwapo wakati huo si sawa na idadi ya watu waliopo sasa. Mahitaji ya ardhi yanaongezeka na si kupungua.

Kuhusu eneo lenye ukubwa wa ekari 10,000 zilizotolewa kwa wananchi na Rais wa Awamu ya Tano katika eneo hilo la Kagera Nkanda, Zitto alimtaka Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jery Silaa kusimamia ahadi hiyo kwa kuhakikisha inawanufaisha wananchi.

Chama hicho pia kimewataka viongozi wote wa chama na serikali waliohusika kukwamisha wananchi kutumia ardhi hiyo wachukuliwe hatua stahiki kwa kuwa wamewafanya wananchi washindwe kutumia ardhi hiyo kuzalisha mahitaji mbalimbali ya kijamii.

Mhifadhi Mkuu Hifadhi ya Msitu wa Makere Kusini, Deograsian Kavishe alisema TFS ndio inasimamia msitu huo. Baadhi ya vijiji vinavyopakana na hiyo hifadhi ni Kagera Nkanda na Mvinza.

Alisema kuwa kijijini Mvinza, kuna maeneo ambayo walikuwa wanafanya kazi ambazo si halali ndani ya hifadhi, akizitaja zinajumuisha uchungaji mifugo na kilimo ambazo wamefanya kwa kipindi kirefu katika eneo hilo wakiwa wavamizi.

Mwaka 2017, Rais John Magufuli (hayati) alitoa maelekezo kwamba wananchi wa vijiji vinavyozunguka Msitu wa Hifadhi ya Makere Kusini hawana ardhi ya kutosha ya kilimo, akatoa maelekezo umegwe ili wagawiwe kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Alisema hekta 5,343 zilikwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kasulu Vijijini na eneo hilo linatumiwa na halmashauri kama chanzo cha mapato kwa kukodisha watu wenye uhaba wa ardhi kwa ekari moja Sh. 50,000 kwa mwaka.

Alifafanua vimetengwa viunga mbalimbali toka kwenye hilo eneo na anayehitaji kutoka nje ya Kasulu na ndani anaweza kupanga akafanya shughuli za kilimo.

Alibainisha kuwa kati ya hizo hekta 10,000 zilizomegwa, hekta 2,374 walipewa Kijiji cha Mvinza ambako walitakiwa wapange matumizi, lakini wakaendelea kubaki kwenye maeneo mengine ambayo sekretarieti haikuyaainisha.

Kwa upande wa Kijiji cha Nkanda, alisema walipata hekta 496, hivyo maeneo hayo yaliyokwenda kwenye vijiji hivyo na wao ndio walikuwa na dhamana ya kuyapangia matumizi.

Kavishe alisema dhana ya kwamba wananchi wamenyang'anywa maeneo na kukodishiwa watu wengine si ya kweli.

KABWELA FADHILI MOHAMED



# FCC yateketeza bidhaa za bil. 10/-

**Na Joseph Mwendapole**

TUME ya Ushindani (FCC) imeteketeza bidhaa hafifu na bandia zenye thamani ya Sh. bilioni 10 kila mwaka.

Hayo yalibainishwa wiki iliyopita na Meneja Ushawishi wa Ushindani wa FCC, Alex Mmbaga alipotoa mada kwenye mkutano wa saba wa Jukwaa la Wahariri (TEF) uliofanyika mkoani Lindi.

Alikuwa anazungumzia mikakati mbalimbali ya FCC kukabiliana na bidhaa bandia na bidhaa hafifu nchini.

Alisema bidhaa zote hizo huteketezwa kwa gharama ya wenye bidhaa na wamekuwa wanawachukua kwenda kushuhudia namna zinavyoteketezwa kama hatua ya kuwafanya wasirudie makosa.

Alisema biashara ya bidhaa bandia ni biashara yenye faida kubwa kwa wafanyabiashara wasio waaminifu, hivyo si rahisi kwao kuiacha.

Alisema mapambano dhidi ya bidhaa bandia yanawagusa watu wenye uwezo mkubwa kifedha, akibainisha kuwa baadhi ya wahalifu waliokuwa wanauza dawa za kulevya wamehamia kwenye biashara hiyo. Ina hatari 'ndogo' kuliko dawa za kulevya.

Alisema kwa kushirikiana na wadau wengine wamefanikiwa kuifanya Tanzania kuwa sehemu salama kwa wawekezaji na walaji na kushauri kuwa kila mamlaka inapaswa kutimiza wajibu wake.

"Bidhaa bandia ni bidhaa zilizotengenezwa kwa kuiga alama ya bidhaa ya mtu mwingine bila ridhaa yake kwa nia ya kumlaghai mlaji na mara nyingi hazina ubora unaotakiwa," alisema Mmgaba.

Alisema FCC imekuwa inaelimisha wafanyabiashara kupitia jumuiya zao na walaji kuhusu matakwa ya Sheria ya Alama za Bidhaa ya Mwaka 1963 kama ilivyorekebishwa pamoja na madhara ya bidhaa hizo kwa jamii na uchumi kwa ujumla.

Alisema katika kutekeleza sheria husika wamekuwa wanashirikiana na wamiliki wa nembo na taasisi zingine za serikani kama vile Mamlaka ya Mapato (TRA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

Alitaja wadau wengine kuwa ni Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Alisema watu wanaojishughusha na bidhaa bandia ni wahalifu, hivyo mara nyingi wamekuwa wanafanya shughuli hizo kwa kujificha na hawalipi kodi serikalini.

Ofisa huyo wa FCC alisema watengenezaji bidhaa bandia hawawajibiki kwa athari zinazoweza kumpata mlaji kwa sababu huwa hajitambulishi kuwa yeye ndiye mtengenezaji wa bidhaa hizo. Mmbaga alisema bidhaa bandia huuzwa kwa bei ambayo ni karibu sawa na bidhaa halisi, hivyo walaji hudanganywa na kuibiwa.

Alisema bidhaa bandia ni bidhaa duni na zina madhara makubwa kwa mlaji, akitolea mfano wa vyakula na dawa ambavyo wakati mwingine vinaweza kusababisha kifo.

Mmbaga alisema bidhaa hizo zinamwondoa kwenye soko mfanyabiashara wa bidhaa halisi kwa sababu zile bandia huuzwa kwa bei ya chini.

Alisema bidhaa bandia hufukuza, kuwaogopesha na kuwatorosha wawekezaji na kuua biashara zilizopo na hivyo kulikosesha taifa mapato, rasilimali na upotevu wa ajira kwa wananchi.

"Anayenunua bidhaa bandia huishia kutumia fedha nyingi zaidi kwa bidhaa ileile kwa sababu uhai wa bidhaa bandia ni mfupi na hivyo kuongeza umaskini.

"Kuna dhana kwamba bidhaa bandia ni nafuu na kwa sababu hiyo inasaidia kulinda maslahi ya maskini na hiyo inaonekana kama ni hoja yenye mantiki, lakini kimsingi haina mashiko kwa sababu atalazimika kununua mara nyingi zaidi ya yule aliyenunua bidhaa halisi," alisema.

Alisema wanashirikiana kikamilifu na wafanyabishara na walaji katika kupambana na bidhaa bandia na hafifu na kufungua zaidi ofisi za kanda ikiwamo mikoa ya Kigoma na Mtwara.

Alisema mpango mwingine ni kuongeza juhudi za kuelimisha wafanyabiashara na walaji kuhusu matakwa ya sheria na madhara ya bidhaa bandia.



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata, akizungumza katika mkutano wa jukwaa la waendesha uchumi walioidhinishwa uliojadili changamoto mbalimbali katika kuboresha kazi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Madereva wanaokiuka sheria za barabarani kufuatiliwa kielektroniki

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, amesema serikali inafanya mchakato wa kuharakisha kuingia katika mfumo unaotumika kutoa faini moja kwa moja kwa madereva wanaochezea mfumo wa ufuatiliaji wa magari (VTS) na kukiuka sheria za barabarani ikiwamo kuendesha kwa mwendokasi.

Kihenzile alitoa kauli hiyo alipotembelea Ofisi za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), jijini Dar es Salaam.

Alisema mfumo huo ni mzuri kwa kuwa ni wa kielektroniki na hutumika nyakati zote, kwenye mvua au usiku.

"Huu mfumo ni mzuri sana kwa sababu ni tofauti na ule wa kusubiri mpaka Trafiki apige tochi, huu wenyewe ukifanya kosa tu au ukiendesha mwendokasi unakupiga faini moja kwa moja tofauti na ule wa sasa ambao ikinyesha mvua kubwa au ni usiku hakuna mtu barabarani wa kusimamia lakini huu wenyewe unafanya kazi muda wote," alisema Kihenzile.

"Mfumo huu utatusaidia sana kupunguza ajali za barabarani na kuwaweka Watanzania wasio na hatia salama. Kwa sasa tunaendelea kuchakata kujua ni namna gani tutautumia, lakini tunaamini kwamba huu ndio utakuwa suluhisho kwa madereva wasio waaminifu."

Aliwaangiza LATRA kuondoa changamoto zote zilizopo kwenye mchakato wa mitihani wa kuwatambua na kuwasajili madereva wanaofanya mitihani hiyo na kufaulu.

"Lakini jambo jingine kwa upande wa LATRA, nimebaini kuna changamoto ya mfumo wa kufanya mitihani, kwa hiyo wameniahidi watajipanga vizuri na ndani ya wiki mbili watakuja na suluhisho," alisema Kihenzile.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Prof. Ahmed Mohamed Ame, alisema endapo mfumo huo utaruhusiwa kuanza kufanya kazi, kuna uwezekano mkubwa wa kudhibiti ajali za barabarani.

"Kama kwa sasa mfumo utaruhusiwa kudhibiti magari yote yanayotumia barabara zetu ikiwamo ya watu binafsi mpaka magari ya serikali, tukaweza kuona mwenendo wao na tabia zao barabarani, tunaamini kwamba kama si kumaliza basi tutapunguza kiwango kikubwa cha ajali za barabari na vifo vya watu ambao hawana hatia," alisema Dk. Ndunguru.

"Tutashukuru sana kama serikali itafika mahali pa kudhibiti magari yote na sisi tuko tayari kusimamia hili kwa sababu uzuri wa huu mfumo utakuwa unatuma moja kwa moja adhabu kwa madereva, bado tunazungumza na Jeshi la Polisi kuona namna ya kuuendesha."

Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara wa Mamlaka hiyo, Johansen Kahatano, alisema tangu waanze kusajili na kuwaingiza kwenye mfumo madereva waliofanya mtihani na kufaulu vizuri, hakuna ambao wamebainika kufanya makosa barabarani mpaka sasa.

## Sababu ujenzi wa shule mpya

**Na James Mwanamyoto**

NAIBU Katibu Mkuu (Elimu), Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Dk. Charles Msonde amesema serikali inajenga shule mpya nchini, ili kutatua changamoto ya watoto kutembea umbali mrefu kufuata elimu na kuondoa msongamano wa wanafunzi darasani.

Dk. Msonde aliyasema hayo jana akiwa wilayani Namtumbo, mkoani Ruvuma wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Mputa inayojengwa kupitia fedha za mradi wa SEQUIP.

Dk. Msonde alisema serikali haijengi shule kwa lengo la kujifurahisha au kumridhisha mtu, bali inajenga shule kwa lengo la kuwawezesha watoto wasitembee umbali mrefu kufuata elimu.

"Lengo ni kuwawezesha watoto wa Kitanzania wanaoingia sekondari kumaliza masomo bila kisingizio cha umbali ili waondoke na ujuzi na umahiri wa kujiletea maendeleo yao pamoja na kuleta maendeleo ya jamii zao na taifa kwa ujumla," Dk. Msonde alisema.

Dk. Msonde alihimiza kuwa serikali ikiongeza fedha za ujenzi wa shule za sekondari, watendaji na viongozi wa kisiasa wajenge shule kwa kuzingatia kigezo cha utatuzi wa changamoto ya umbali na msongamano wa wanafunzi darasani na kwenye mabweni.

Vilevile, Dk. Msonde aliupongeza uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kwa kuchagua eneo zuri la kujenga Shule ya Sekondari Mputa na kuongeza kuwa ujenzi wake ukikamilika vizuri, inaweza kuongezwa adhi ya kuwa na kidato cha tano na cha sita.

Akitoa taarifa ya ujenzi kwa Dk. Msonde, Mkuu wa Shule ya Sekondari Mputa, Godlove Chumi alisema ujenzi umefikia asilimia 71 na mafundi wanaendelea kujenga giblo, kupiga plasta, kufunga bodi ya juu (gypsum board), kupiga koplo na kupachika fremu za mirango.

Kwa niaba ya bodi ya shule, Kamati ya Ujenzi, viongozi na jumuiya nzima ya Kata ya Mputa, Chumi aliishukuru serikali kutoa fedha ambazo zinatumika kujenga miundombinu ya Shule ya Sekondari Mputa.

Sh. 560,552,827 zimetolewa na serikali kupitia mradi wa SEQUIP kwa ajili ya ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Mputa. Hadi jana, Sh. 379,932,683 zilikuwa zimeshatumika na kiasi kilichosalia kwa ajili ya kukamilisha ujenzi ni Sh. 180,620,144.



## Kijaji apongezwa kuleta mageuzi TANAPA

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), limemuaga rasmi aliyekuwa Kamishna wa Uhifadhi, Dk. Allan Kijazi baada ya kuhitimisha utumishi wake katika shirika hilo baada ya kulitumikia kwa miaka 11.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa TANAPA, Jenerali Mstaafu George Waitara, alimpongeza Kamishna Mstaafu Kijazi kwa kuleta mageuzi katika shirika hilo ikiwamo falsafa ya uhifadhi kwa kubadili muundo wa utendaji hadi kuwa mfumo wa jeshi usu ambao umeongeza uwajibikaji na kupunguza ujangili nchini.

"Nakupongeza sana kwa kustaafu kwa heshima kwani ulifanya kazi usiku na mchana kwa bidii, uliweza kushauri bodi vizuri kuhusu shirika na umekuwa ukijali maslahi ya watumishi na maendeleo kwa ujumla," alisema.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Kijazi aliwashukuru marais wa awamu zote alioshirikiana nao wakati wa utekelezaji wa majukumu yake huku akiwataka watumishi wa TANAPA kuendelea kudumisha umoja na kuongeza bidii kazini.

Alisema haikuwa rahisi kufanya kazi na marais watatu, mawaziri sita ambao kila mmoja alikuwa anaingia na mtazamo wake ila aliweza kutokana na ushirikiano ambao umewezesha shirika hilo kuendelea kung'aa.

Dk. Kijazi alisema kipekee anamshukuru Rais wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli kwa kuendelea kumwamini na kumteua hasa kipindi cha mabadiliko ya muundo wa shirika kutoka muundo wa kiraia hadi kuwa muundo wa kijeshi.

Akizungumza kwa niaba ya wadau wa utalii, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Wenye kampuni za utalii Tanzania (TATO), Cyril Akko, alitoa pongezi kwa Dk. Kijazi kwa utumishi wake na kuwa aliweza kuwa daraja kati ya sekta binafsi na uhifadhi, iliyowezesha kukuza sekta hiyo muhimu ya utalii.

**"Nakupongeza sana kwa kustaafu kwa heshima kwani ulifanya kazi usiku na mchana kwa bidii, uliweza kushauri bodi vizuri kuhusu shirika na umekuwa ukijali maslahi ya watumishi na maendeleo kwa ujumla," alisema.**

# Huduma rasmi za fedha bado changamoto kwa Watanzania

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KAMISHNA wa Uendelezaji Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Dk. Charles Mwamwaja, amesema kuwa kulingana na utafiti walioufanya hivi karibuni takwimu zinaonyesha kuwa asilimia kubwa ya Watanzania bado hawajafikiwa na huduma rasmi za kifedha.

Hayo aliyasema wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya tatu ya wiki ya huduma za kifedha yanayoendelea jijini Arusha katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid na yatafikia tamati Novemba 26, mwaka huu.

Dk. Mwamwaja alisema hadi sasa ni asilimia 53.8 ya Watanzania ndio wamefikiwa na huduma za fedha tofauti na malengo ya taifa yanayohitaji hadi kufikia mwaka 2025 asilimia 80 wawe wamefikia hivyo kazi kubwa inahitaji kufanyika ili kuziba pengo hilo.

"Tunaposema huduma rasmi za kifedha ni zile ambazo zinahusisha mifumo rasmi ya kifedha ikiwamo huduma za kibenki, masoko ya dhamana na mitaji, bima na mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi," alisema.

Alisema serikali imekuwa ikiweka mazingira wezeshi ya kisera, kikanuni na kutoa miongozo mbalimbali katika kuwezesha utoaji wa huduma za fedha hapa nchini ili kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa.

Akizungumzia maadhimisho hayo, Dk. Mwamwaja alisema yameandaliwa na kuratibiwa na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na wadau wa sekta za fedha na jumla ya benki 35 zitashiriki kwenye maadhimisho hayo.

Alisema agenda yao kuu itakayoongoza shughuli hiyo ni kutoa elimu kwa wananchi ili kujenga uelewa na waweze kutumia huduma za kifedha kwa namna ambayo ni sahihi.

Pia alisema lengo lingine la maadhimisho hayo ni wananchi kutambua fursa zinazotolewa kwenye sekta ya fedha kwa kuwa takwimu zinaonyesha asilimia kubwa ya Watanzania bado hawajafikiwa na huduma rasmi za kifedha. Meneja Msaidizi Kitengo cha Mawasiliano, Benki Kuu ya Tanzania(BoT), Novess Mosses, alisema benki hiyo imeshiriki kwenye maadhimisho hayo ili kutoa elimu kwa wananchi namna ya kutumia huduma za kibenki kwenye taasisi za kifedha.

Aidha, alisema wanaamini kuwa endapo wananchi wanapata uelewa wa namna ya kutumia huduma hiyo na kutambua wajibu wao itasaidia kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (katikati), akizungumza baada ya kutembelea mgodi wa madini ya Tanzanite kitalu C unaomilikiwa na Kampuni ya Franone Mining Ltd katika Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro mkoani Manyara juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Onesmo Mbise. **PICHA: GIFT THADEY**

# Katibu Mkuu aagiza kuzalishwa wataalamu zaidi kinywa, meno

**Na Oscar Assenga,** TANGA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Idara ya Afya, Dk. Wilson Mahera, ameviagiza vyuo vya afya ambavyo havina kozi ya Shahada ya Udaktari wa Kinywa na Meno kuanzisha ili kuongeza upatikanaji wa madaktari wa kada hiyo nchini.

Dk. Mahera aliyasema hayo jana jijini Tanga wakati akifungua Mkutano wa Madaktari wa Kinywa na Meno Tanzania Kitaifa unaofanyika mkoani hapa ambapo alisema kwamba atafikisha ujumbe huo kwa wakuu wa vyuo hivyo hapa nchini.

Alisema kwa kufanya hivyo kutawezesha upatikanaji wataalamu wengi ambao watasaidia katika utoaji huduma kwa wananchi wanaokumbana na changamoto mbalimbali za afya ya kinywa na meno hapa nchini.

"Kupitia mkutano huu niagize vyuo vya Afya nchini ambavyo havina kozi ya Shahada ya Udaktari wa Kinywa na Meno kuanzisha ili kusaidia kuongeza upatikanaji wa wataalamu hao hapa nchini," alisema Dk. Mahera.

Katika mwaka 2022 kitaifa kulikuwa na wagonjwa wa kinywa 747,485 ambapo waliooza meno 522,777 sawa na asilimia 68.9 ya wagonjwa wote wa kinywa na meno na waliokuwa na matatizo ya fizi ni 78,755.

Alisema kwa takwimu hizo tatizo la kuoza kwa meno bado ni kubwa hapa nchini bado na wana kazi kubwa ya kufanya wagonjwa 156,576 sawa na asilimia 30 walioza meno yalizibwa na wagonjwa 265,249 sawa 49.6 na asilimia walioza meno yaling'olewa.

"Tatizo la meno likikupata ukiamka asubuhi unang'olewa, niwatake wataalamu mjikite zaidi kutibu na sio kuyang'oa kwa maana serikali imewekeza miundombinu yote wezeshi kuhakikisha wananchi wanapatiwa tiba ya meno na sio kung'oa jino," alisema. Alisema pia kuna maeneo huduma za kinywa na meno hazipatikani na kusababisha wananchi kutembelea umbali mrefu kufuata huduma hiyo jambo ambalo si sahihi.

Aidha, aliagiza na kuwaelekeza waganga wakuu wa mikoa na halmashauri kuhakikisha vituo vya afya vya kimkakati na visivyo vya kimkakati vinaanza kutoa huduma hiyo ili kuepusha wananchi kutembelea umbali mrefu.

Aliwataka pia kuwa na vifaa stahiki kama vile viti vya kutolea huduma na vifaa vya kisasa na mashine za kifanyia uchunguzi wa afya ya kinywa na meno kulingana na miongozo inayotolewa na Wizara ya Afya.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dk. Japhet Simeo, alisema mkoa huo upo salama na kuwasihi wajumbe kuhakikisha wanakuwa makini vitu ambavyo vitawasilishwa kwenye mkutano huo.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Kinywa na Meno kutoka Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, alisema kikao hicho kitaleta mapinduzi makubwa kwenye sekta hiyo.

Alisema Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI wamekuwa wakiratibu vikao hivyo na kuna baadhi yao hawatilii mkazo vikao uamuzi kwa kumwomba katibu mkuu kuanza kuwachukulia hatua watu wote wanaokaidi wito wa kuhudhuria.

"Nikuombe ikikupendeza uwachukulie hatua kwani maendeleo hayawezi kupatikana kama watu wana puuzia vikao vya msingi vya kisekta ambavyo vinaleta mabadiliko katika kutoa huduma bora ya kinywa na meno. Ofisi hii iliandikia Halmashauri 36 kuleta wataalamu ngazi ya Halmashauri lakini mpaka leo wamefika 17," alisema.





# Wakulima Ngara washtuka parachichi kutoka Burundi zinavyoua soko

**Na Jenesta Jasson,**
NGARA

WAKULIMA wa parachichi wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera wamelalamikia kupata hasara baada ya kushuka kwa soko la zao hilo kunakosababishwa na uingizaji wa parachichi kutoka nchini Burundi.

Walisema uingizwaji wa tunda hilo kutoka nchini Burudi kumeshusha bei ya zao hilo nchini kutoka Sh.75,000 kwa gunia hadi kufikia Sh.35,000 hali inayowasababishia hasara.

Wakulima hao walitoa kilio chao kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza na Nipashe na kuiomba serikali kuweka udhibiti katika uingizwaji wa zao hilo nchini ili kuwasaidia kuendelea na biashara hiyo.

Mwenyekiti wa Wakulima hao Wilaya ya Ngara, Ahmad Fadhili, aliiomba serikali kuweka utaratibu maalumu kwa wafanyabiashara wanaoingiza zao hilo nchini ikiwa ni pamoja na kutafuta masoka ya zao hilo ili kuwasaidia wakulima hao kuendelea na kilimo hicho. Vilevile aliomba kuwasaidia wakulima vitendea kazi pamoja na kujenga viwanda vya uchakataji vitakavyoongeza uhitaji wa zao hilo ili kurejesha thamani yake na kuwasaidia wakulima kukabiliana na hasara wanazokumbana nazo kwa kipindi hiki wanaposhindana kibiashara na wenzao wa Burundi.

Katibu wa chama cha wakulima wa zao hilo ambaye pia ni Mkulima,Godfrey Nyange, alisema soko kwa sasa limekuwa gumu kwani parachichi nyingi zinatoka Burundi hivyo kusababisha bei kushuka bila kujali gharama zilizotumika katika kilimo hicho.

Mkulima mwingine, Brasio Daniel aliiomba serikali kupitia wizara ya kilimo kuwasaidi wakulima hao pembejeo ikiwa ni pamoja na mbolea ili waweze kuendesha shughuli zao kwa ufanisi na kuinua uchumi wao binafsi na kuongeza pato la Taifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, Solomon Kimilike, aliwataka wakulima hao kutokuwa na wasiwasi kwa kuwa kupitia baraza la madiwani wameahidi kuwapa kipaumbele wakulima hao na kulifanya zao hilo kuwa endelevu ndani ya wilaya.

Alisema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 zimetengwa Sh.milioni 100 kuhakikisha wakulima hao wanapatiwa miche ya kutosha na kuboresha kilimo chao.

Kuhusu uingizwaji wa parachichi nchini zinazotokea Burundi serikali italifanyia kazi kwa kutazama namna nzuri ya kudhibiti bei zake na kuweka usawa kwa wafanyabiashara wote..



Wafanyakazi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), wakitandaza mabomba ya maji katika Kijiji cha Mkirira, Musoma Vijijini mkoani Mara mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi 88,000 kupatiwa kinga ya kichocho, minyoo Sengerema

**Na Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

ZAIDI ya wanafunzi 88,000 wenye umri wa miaka mitano hadi 14 wa shule za msingi 111 wanatarajiwa kupata dawa ya kinga ya magonjwa ya kichocho na minyoo ya tumbo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza.

Utolewaji wa dawa hizo unatarajiwa kufanyika kuanzia kesho Novemba 23 na 24, 2023 ili kukabiliana na magonjwa hayo hatari kwa watoto husussani katika kipindi hiki cha mvua.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Dk.Fredrick Mugarula, alisema dawa zitakazotolewa ni za kawaida na zimekuwa zikitolewa mara kwa mara hivyo kuwataka wajumbe wa kikao cha maandalizi kupeleka elimu katika jamii ili kufanikisha utolewaji wa kinga hiyo.

Dk. Mugarula aliwaondoa hofu wananchi na kuwataka kutokuzitilia shaka dawa hizo kwani ni zilezile zinazotumika katika zahanati, vituo vya afya , hospitali na kwenye maduka ya dawa zikilenga kuwakinga watoto wote wenye umri wa miaka Mitano hadi 14.

Mratibu wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele, Rachel Ntegwisangu, alisema shule kutoka kata 22 zitapatiwa dawa ya kichocho na dawa ya minyoo ya tumbo huku shule zilizobaki kutoka katika Kata 4 zitapata dawa za minyoo ya tumbo pekee kutokana na hesabu ya dawa hizo.

Rachel alizitaka shule zote za msingi kuhakikisha wanaandaa chakula kwaajili ya wanafunzi wote na kuhakikisha wanakula kabla ya matumizi ya dawa hizo.

Mchungaji wa kanisa la AICT MLIMANI na mjumbe wa kikao cha uhamasishaji ,Amos Ndugwa aliomba uongozi wa ofisi ya Mganga Mkuu wa Halmashauri kuhakikisha walengwa wote wanapatiwa dawa hizo ili kuhakikisha magonjwa hayo yanadhibitiwa.

# Wajawazito waomba vifaa kudhibiti vifo watoto njiti

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAJAWAZITO katika Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kusambaza vifaa tiba vya kutunza watoto wanaozaliwa kabla ya kutimiza miezi tisa (njiti) kwenye zahanati na vituo vya afya vilivyopo pembezoni mwa miji ili kupunguza vifo vya watoto wachanga .

Ombi hilo lilitolewa juzi katika hafla ya utoaji wa elimu ya afya ya uzazi kwa wajawazito na wanawake wenye watoto njiti iliyofanyika katika Kituo cha Afya Bugarama ikiwa na dhima ya kuzuia ongezeko na vifo kwa watoto chini ya miezi sita.

Mkazi wa Bugarama, Ester Mathias, alisema wajawazito wengi wanaojifungua watoto njiti wanaotoka vijijini hivyo wanakosa fursa ya kupata huduma bora kwa kuwa hakuna ukosefu wa vifaa tiba vikiwamo vya kutunzia watoto katika vituo vya afya.

Alisema kufuatia tatizo hilo watoto wengi wanaozaliwa chini ya umri wamekuwa wakipoteza maisha kutokana na kukosa huduma stahiki katika vituo vya Afya na zahanati vilivyopo katika maeneo yao na kuomba serikali kuweka vifaa vya kutunzia watoto njiti kuokoa maisha yao.

"Huduma ya kutunza watoto njiti inapatikana Hospitali ya Manispaa ya Kahama pekee ambapo ipo umbali wa kilomita 70 kutoka hapa kata ya Bugarama, tunapojifungua watoto hawa tunalazimika kutumia gharama kubwa za usafiri na kukaa Kahama na wasiokuwa na uwezo wanapoteza vichanga vyao,"alisema Mathiasi.

Muuguzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Nyabulemo Rashidi alisema, wajawazito wengi wanaojifungua watoto njiti huwa na maambukizi ya magonjwa mbalimbali kama vile, UTI sugu, malaria, upungufu wa damu na kufanya kazi nzito bila kupumzika hasa za kilimo shambani.

Kaimu Mganga Mfawidi wa kituo cha afya Bugarama, Cleofas Mganda akitoa taarifa ya upatikanaji wa huduma za afya alisema, kipindi cha Januari hadi Novemba mwaka huu wajawazito 2,534 walijifungua salama huku watoto njiti walikuwa 58 na vifo vya watoto wenye umri chini ya mwezi mmoja vikiwa sita.

Mbunge wa Viti maalum Mkoa wa Shinyanga kupitia Chama cha Mapinduzi(CCM) Santiel Kirumba alisema, serikali kupitia Wizara ya Afya imenunua vifaa tiba kwa ajili ya Watoto njiti na kuvisambaza Hospitali za wilaya na mikoa nchi nzima ili kuhakikisha Watoto wanaozaliwa na tatizo hilo wanapata msaada.

Alisema, wakati serikali ikiendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya afya katika kutatua changamoto za ukosefu wa vifaa hivyo ngazi za zahanati na vituo vya afya ni vema wananchi wakaendelea kupata huduma hizo katika hospitali za Wilaya na mikoa na hiyo ndio sababu ya serikali kujenga hospitali za wilaya kila halmashauri.



Ukurasa 12

## Tanzania sasa kutumia ubobevu wa Vietnam kupata mageuzi kiuchumi



Ukurasa 13

## Uchaguzi unanukia NEC, wadau pamoja majaribio daftari la wapigakura 2025


# siasa

JUMATANO NOVEMBA 22, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


# UWT ina ndoto kuunganisha wanawake bila kujali itikadi kumchagua Rais Samia 2025

## •Yaanzisha kampeni kulinda nafasi adhimu baada ya miaka 60 ya Uhuru

**Na Sabato Kasika**

TANZANIA kwa miaka 60 ya uhuru haikuwahi kuwa na rais mwanamama. Lakini,safari hii nafasi hiyo inashikiliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, hivyo maadamu imepatikana ni kazi ya wanawake kuilinda kwa kumuunga mkono na kwa ujumla kumpa kura ya ndiyo 2025, ili aedelee kuongoza nchi. Anasema Mary Chatanda, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake (UWT).

Anasema wakati taifa likielekea kwenye uchaguzi mkuu wa 2025, UWT wana kampeni maalum, inayowashirikisha wanawake wa Tanzania bila kujali vyama vyao vya siasa na itikadi zke kuhakikisha wote wanampigia kura ya ndiyo Rais Samia, aendelee kuongoza kwa miaka mingine mitano.



Mary Chatanda Mwenyekiti wa UWT. **PICHA: MWANDISHI WETU**

Katika mazungumzo yake na Nipashe jijini Dar es Salaam, anatangaza rasmi kuwa ameanza kuunganisha wanawake ili wawe na kauli moja ambayo ni kumchagua Rais Samia kwa kishindo 2025.

"Mwisho wa uchaguzi ni mwanzo wa uchaguzi mwingine, hivyo tunapomaliza uchaguzi, tunapaswa kujiandaa, kwa mwingine, nami nimeshaanza maandalizi ya kumrudisha Samia kwa kishindo kwa kampeni ya kuunganisha wanawake wenzangu wa Bara na Visiwani," anasema Mary.

Anaonyesha kuwa 2025 si mbali, na kwamba ni muhimu kuwaandaa wapigakura kuwa tayari kushiriki katika uchaguzi na hasa wanawake, kwa maelezo kwamba mwaka huo wanawake wana jambo lao, kama anavyoeleza katika mahojiano haya....

**SWALI:** Kwa nini umeamua kuja na kampeni ya kuunganisha wanawake wote bila kujali vyama vyao wampe kura Rais Samia badala ya kuhamasisha wa chama chako. Msukumo wako ni upi?

**JIBU:** Kwanza ieleweke kwamba, kwa miaka mingi wanawake tumekuwa nyuma katika nafasi za uongozi, hicho ni kilio cha wanawake wote bila kujali vyama wanavyotoka. Hiyo ni ajenda kuu ambayo imekuwa ikikutanisha wanawake pamoja. Lakini pia fursa za uongozi wa juu hasa kwa wanawake ni nadra kutokea kwa mwanamke, hivyo, nafasi iliyopatikana kwetu sisi wanawake baada ya kupata rais mwanamke isiachwe ipite, badala yake tumuunge mkono mwanamke mwenzetu ambaye ameonyesha uwezo mkubwa wa uongozi, tofauti na wengine walivyokuwa wanamchukulia. Niseme kuwa safari hii tumeashaamua Samia arudi katika urais wa mwaka 2025.

**SWALI:** Unatumia mbinu zipi kuwakutanisha wanawake kutoka vyama mbalimbali vya siasa na kufanya kampeni hiyo?

**JIBU:** Ninaongea na viongozi wanawake wa vyama vya siasa kwa njia ya simu, lakini pia kwa kukutana nao, katika vikao mbalimbali vinavyohusu ajenda ya mwanamke na wote tumeshaazimia kwamba hatutaki kumpoteza Samia kwani amefanya makubwa, lakini pia akiwapa kipaumbele wanawake katika uongozi, kujenga sekondari ya wasichana kila mkoa, na mengine mengi bila kusahau kuwarudisha shuleni mabinti walioshindwa kwa sababu mbalimbali.

**SWALI:** Una muda gani tangu uanze kampeni hii na mwitikio ya wanawake kutoka vyama vingine na wasio na vyama ukoje?

**JIBU:** Suala la kampeni nilishaanza muda mrefu na inaendelea kwa kuwakutanisha wanawake wanasiasa katika mijadala mbalimbali na wameonyesha ukubali, kwani wote agenda yetu ni moja ya kumnyanyua mwanamke, hivyo ninaamini tutafanikiwa. Safari hii tunataka kuiondoa dhana iliojenga kwamba wanawake hatupendani.

**SWALI:** Makubaliano katika kampeni yako na wanawake wenzio kutoka vyama vingine vya siasa yakoje? Ina maana wataachana na vyama vyao waungane na CCM. Fafanua kuhusu kampeni hiyo na jinsi ambavyo mtaweza kuifanikisha kama wanawake.

**JIBU:** Jambo ambalo tumekubaliana na kwamba kwenye urais, wote tumpe Rais Samia, lakini katika nafasi nyingine za ubunge na udiwani, kila mmoja wetu kila mmoja awanie katika chama chake kama kawaida, kwenye urais tuonyeshe umoja wetu kama wanawake wa Kitanzania bila kujali vyama na kumchagua Rais Samia. Hivyo, hatutaki vyama vitutenganishe kwenye ajenda hii muhimu. Hatukuwahi kuwa na rais mwanamke na sasa tumempata, hatuna budi kumuunga mkono.

**SWALI:** Kwa upande wa wanawake wanasiasa umeeleza jinsi unavyokutana nao na kuweka mikakati ya kuhakikisha Rais Samia anashinda uchaguzi mkuu 2025, kinamama ambao si wanasiasa unakutana nao, kwa njia ngani?

**JIBU:** Hao nao ninaitisha mikutano na kuzungumza nao. Kwa mfano, wiki hii nitakutana na wanawake makandarasi jijini Dodoma, kuwaeleza dhamira ya wanawake wenzao katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, ili

INAENDELEA UK. 14

# Tanzania sasa kutumia ubobevu wa Vietnam kupata mageuzi kiuchumi

## •Ni mpango wa CCM na Chama cha Kikomunisti



Katibu Mkuu wa CCM Daniel Chongolo na mjumbe wa Kamati Kuu ya CPV Profesa Le Hai Binh. **PICHA: CCM**

**Na Halfani Chusi**

CHAMA cha Kikomunisti cha Vietnam (CPV) na CCM vimetanua wigo wa ushirikiano vikitamani kilichoinua uchumi wa Vietnam kisaidie kuongeza kasi ya maendeleo ya Watanzania.

Kilimo, kinapewa upendeleo na vyama hivyo, kwanza vikikubaliana kushirikiana kwenye nyanja mbalimbali na muhimu ni kuongeza thamani ya kilimo kwenye maeneo ambayo nchi hiyo ya Asia ya Kusini ina uzoefu nayo.

CCM inaomba ushirikiano katika kilimo cha mpunga ili kuwawezesha wakulima kuzalisha mchele kwa wingi utakaoteka soko la ndani na nje.

Aidha, kahawa nayo inaitajwa, ambapo wadau hao wanaeleza kuwa hayo ndiyo mazao yaliyoiletea Vietnam mafanikio kiuchumi na kimaendeleo.

Yanajiri katika kikao kati ya Katibu Mkuu wa CCM Daniel Chongolo, na mjumbe wa Kamati Kuu ya CPV Profesa Le Hai Binh, jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Anaongeza kuwa ndani ya miaka 25 iliyopita uchumi wa Vietnam umekua kwa kasi, ambapo kwa sasa thamani ya fedha za mazao inayouza nje imefikia Dola za Marekani Bilioni 20.

Anaisifu kuwa ni mmoja wa wazalishaji wakubwa wa mchele na kahawa duniani na kwamba mnamo miaka ya 1990 na sasa inashika nafasi ya pili kwa kuuza mchele nje na namba tatu kwa kuuza kahawa.

Vietnam kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia (WB) uchumi wake unakua kwa kasi ukipewa jina la tiger cub' kuwa una nguvu na misuli imara kama mnyama ' kinda la duma au tiger) ikiwa ni pamoja na nchi za Indonesia, Malaysia, Filipino na Thailand.

"Haya ndiyo tunataka tujifunze, tubadilishane uzoefu, mafunzo na hata nyenzo ili Tanzania isonge mbele zaidi," anasema Chongolo

Anamwmabia kuwa kukamilika kwa mpango huo kutaibua neema kwa wakulima, kwani kupitia muunganiko huo watapata wataalamu kutoka Vietnam na uzoefu mkubwa kwenye sekta ya kilimo ambacho ndiyo nyenzo kuu ya ukuaji wa uchumi nchini.

> "Urafiki wetu huu wa kihistoria ambao umekuwa sawa na undugu, umekuwa ni wa nyakati zote na majira yote, kisiasa, kiuchumi na kijamii, ukijengwa katika misingi ya itikadi na falsafa za tangu waasisi wa vyama hivi na mataifa haya mawili." anasema

Chongolo anabainisha kuwa CCM, inaridhishwa na urafiki na uhusiano wake na chama cha CPV na kwamba kipo tayari kuendeleza ushirikiano kati ya pande hizo mbili ili kuongeza fursa kwa Watanzania kunufaika zaidi, kupitia nyanja za sayansi na teknolojia, kukuza uzalishaji na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo ambako Vietnam ina uzoefu mkubwa.

Akiwa katika makao makuu ya CCM, Chongolo anamwambia mjumbe wa Kamati Kuu ya CPV Profesa Binh akimuomba pia ushirikiano katika eneo la sayansi na teknolojia.

Kwenye kikao hicho katibu huyo anaahidi kwamba kupitia mahusiano ya kihistoria kati ya CCM na CPV, kisiasa, kijamii na kiuchumi, vyama hivyo vitaimarisha zaidi misingi itakayotumiwa na Serikali za nchi zote mbili.

"Kama ulivyosema Profesa Binh, kuhusu kupandisha hadhi ya urafiki, ushirikiano na uhusiano wetu huu, CCM iko tayari, kama ambavyo ninyi mko tayari.

"Urafiki wetu huu wa kihistoria ambao umekuwa sawa na undugu, umekuwa ni wa nyakati zote na majira yote, kisiasa, kiuchumi na kijamii, ukijengwa katika misingi ya itikadi na falsafa za tangu waasisi wa vyama hivi na mataifa haya mawili." anasema

Anamweleza mjumbe huyo kuwa ni muhimu sasa tija iende mbali na kuonekana dhahiri katika kusaidia kubadilisha hali za maisha ya wananchi waliovipatia vyama hivyo, ridhaa na dhamana ya kuongoza. Katika eneo hilo la uzalishaji Vietnam imepiga hatua kubwa na ina uzoefu mkubwa.

Aidha, kuhusu matumizi ya sayansi na teknolojia pia wamekwenda mbali kwamba hata kilimo na mnyororo wake thamani sayansi na teknolojia imechukua nafasi kubwa ili kuwa na uzalishaji na thamani zaidi akisema Tanzania inayo mengi ya kujifunza kutoka Vietnam.

Anaongeza: "Serikali za CCM zote mbili, ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wa CCM na ile ya Mapinduzi Zanzibar, inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, zimeweka mikakati na msukumo mkubwa na katika eneo la uzalishaji, katika sekta zote, kama kilimo, ili kukuza na kuimarisha uchumi." Anasema Chongolo.

Anasema hayo ndiyo Tanzania inataka kujifunza, kubadilishana uzoefu, mafunzo na hata nyenzo ili nchi na watu wake wapige hatua mbele zaidi kupitia uzalishaji wenye tija.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama tawala cha Vietnam Profesa Binh, anasema thamani ya CCM, serikali yake na Tanzania kwa ujumla mbele ya CPV na Vietnam, ni kubwa mno kwa sababu za kihistoria, ambapo vyama hivyo na nchi zote mbili zina mtazamo mmoja wa itikadi ya kisiasa na kiuchumi, na historia imewapitisha katika ushirikiano wa mapambano ya watu wanyonge kujikomboa.

"Kitu kingine ambacho nchi zetu chini ya CCM na CPV vinaweza kujivunia na kugeuza kuwa ni fursa kwa kila moja kunufaika, ni kuwa katika maeneo mazuri kijiografia. Tanzania ni lango la nchi nyingi za Afrika kwenye usafirishaji. Hivyo hivyo, kijiografia Vietnam iko katika eneo ambalo ni lango kwa nchi nyingi za Asia.

"Hii ni fursa kwa wote kushirikiana. Tuko tayari kupandisha hadhi ya urafiki na ushirikiano wetu kati ya CCM na CPV kwa ajili ya Tanzania na Vietnam ili tusaidiane katika kuongeza uzalishaji, kukuza uchumi na pato la mtu na kuboresha hali za maisha ya watu wetu," amesema Prof. Le Hai Binh.

Anasema ni hatua nzuri kwa chama tawala, hali hiyo italisaidia taifa kupiga hatua kwenye maeneo ya kilimo akisema ni jambo linalopaswa kuigwa kuiletea nchi na wanachama wake manufaa endelevu.

# Uchaguzi unanukia NEC, wadau pamoja majaribio daftari la wapigakura 2025



Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Ramadhani Kailima, akiwasilisha mada kwenye mkutano wa wadau wa uchaguzi jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: NEC**

**Na Abdulwakil Saiboko**

UHURU wa kutoingiliwa katika utekelezaji wa majukumu na wa kufanya maamuzi ni nguzo muhimu kwa refa anapokuwa anachezesha mpira uwanjani, ndiyo unaomfanya kuwa na sauti ya mwisho pale anapoamua jambo na maamuzi yake hayawezi kuingiliwa na wachezaji, benchi la ufundi, mashabiki au watazamaji.

Huu ni mfano unaosadifu namna ambavyo Tume ya Taifa ya Uchaguzi(NEC) imepewa uhuru wa kutekeleza majukumu na kujiamulia mambo yake bila kuingiliwa, ni katika ibara ya 74(7) na (11) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

"Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake yaliyoainishwa katika ibara hii, Tume ya Uchaguzi itakuwa ni idara huru inayojitegemea, itafanya maamuzi yake rasmi kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa vikao, na mtendaji wake mkuu atakuwa ni Mkurugenzi wa Uchaguzi ambaye atateuliwa na kufanya kazi kwa mujibu wa masharti ya sheria iliyotungwa na bunge," ibara ya 74(7) inasema.

Aidha, ibara ya 74(11) ya katiba hiyo inaelekeza kuwa katika kutekeleza madaraka yake NEC haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya serikali, au maoni ya chama chochote cha siasa".

Kwa kuwa msingi wa uhuru wa taasisi unajengwa na katiba inathibitisha bila shaka kwamba NEC iko huru na kwamba haingiliwi na mamlaka nyingine. Hata hivyo, pamoja na uhuru huo, bado imekuwa ikiwashirikisha wadau mara kwa mara hasa pale inapotekeleza majukumu yake.

> "Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake yaliyoainishwa katika ibara hii, Tume ya Uchaguzi itakuwa ni idara huru inayojitegemea, itafanya maamuzi yake rasmi kuhusu utekelezaji...

Majukumu ya tume kama yanavyoainishwa na katiba ni kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura katika uchaguzi wa rais na wabunge wa Jamhuri ya Muungano na madiwani Tanzania Bara, kuchunguza mipaka na kugawa maeneo mbalimbali ya uchaguzi wa wabunge, kusimamia na kutekeleza majukumu mengine ya kisheria.

Majukumu mengine ya chombo hicho kwa mujibu wa kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, sura ya 343, na kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, sura ya 292 ni pamoja na kutoa elimu ya mpigakura nchi nzima, kuratibu na kusimamia watu wanaotoa elimu hiyo na kuteua na kuwatangaza wabunge na madiwani wanawake wa viti maalum, kwa mujibu wa ibara ya 78(1) ya katiba ya Tanzania.

Tume katika utaratibu iliyojiwekea wa kukutana na wadau wake, kuwajulisha juu ya utekezaji wa majukumu yake na kupata maoni yao, hivi karibuni inakutana nao kwenye mikutano miwili ya kitaifa inayofanyika Dar es Salaam na miwili katika ngazi ya mkoa huko Mara na Tabora.

Mikutano hiyo inalenga kuwajulisha wadau wa uchaguzi kuhusu majaribio ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura yanayofanyika kata ya Ikoma Wilaya ya Rorya mkoa wa Mara na ile ya Ng'ambo iliyopo Manispaa ya Tabora kuanzia Novemba 24 hadi 30 2023.

Wanaokutana na tume ni pamoja na viongozi wa vyama vya siasa, asasi za kiraia, viongozi wa dini, wahariri wa vyombo vya habari, wawakilishi wa asasi za watu wenye ulemavu, wanawake, vijana na wazee wa kimila. Ikumbukwe kwamba ni utaratibu wa tume kuwashirikisha wadau hawa licha ya uhuru iliyopewa na katiba jambo ambalo linadhihirisha utayari wa chombo hiki kilichopewa dhamana ya kusimamia ustawi wa demokrasia nchini kupokea maoni na ushauri kutoka kwa wananchi kinaowahudumia.

Akiwasilisha mada kwenye mikutano hiyo ya wadau, Mkurugenzi wa Uchaguzi Ramadhani Kailima anasema majaribio ya uboreshaji wa daftari la wapigakura ni maandalizi ya kuanza kwa uboreshaji wa daftari hilo utakaofanyika nchi nzima kwa utaratibu na muda utakaotangazwa na tume.

Kailima anasema madhumuni ya majaribio hayo ni kupima uwezo na ufanisi wa vifaa vya uandikishaji vitakavyotumika wakati wa uboreshaji, kupima uwezo na ufanisi wa mfumo wa uandikishaji wa wapiga kura ulioboreshwa na kubaini iwapo kutajitokeza mapungufu ili yafanyiwe kazi kabla ya uboreshaji rasmi kuanza.

Majaribio hayo yatahusisha vituo 16 vya kuandikisha wapiga kura. Kati ya hivyo, vituo 10 vipo katika kata ya Ng'ambo na vituo sita vipo kata ya Ikoma, wakati vituo vya uandikishaji vitafunguliwa saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni.

"Changamoto zitakazobainika katika zoezi hilo, zitaiwezesha tume kujipanga vyema katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura awamu ya kwanza unaotarajiwa kuanza 2024....".

Akizungumza kuhusu teknolojia itakayotumika na ambayo inafanyiwa majaribio ili kubaini uwezo na changamoto zake, anasema NEC itatumia BVR Kits mpya tofauti na zilizotumika mwaka 2015, 2019 na 2020, akiongeza kuwa BVR Kits za miaka iliyopita mbali ya kutumia program ya window, pia zilikuwa na uzito wa kilo 35 tofauti na zitakazotumika katika majaribio ya sasa zinazotumia program ya 'android' na zina uzito wa kilo 15 ambao ni zaidi ya nusu ya uzito wa zile za zamani.

Android ni mfumo wa kisasa wa kielektroniki wa kuendesha simu za mkononi au vishkwambi (tablets) unaotumia zaidi kugusa 'skrini' au kioo chake badala ya mfumo wa zamani wa kubonyeza herufu kila unapotaka kuitumia.

BVR Kits hizo licha ya kuwa na uzito mdogo, zinabebeka kwa urahisi, zina mfumo wa uandikishaji wa wapiga kura ambao umesanifiwa na kuboreshwa ili kuendana na BVR Kits za sasa, akiwaeleza wadau hao wa uchaguzi kuwa Tume imezichagua kata hizo mbili kwa kigezo cha ongezeko la watu kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya 2022, hali ya miundombinu ya mawasiliano na hali ya mazingira na mwingiliano wa watu kutoka nchi jirani kwa maeneo ya mipakani.

Anaifafanua kwamba majaribio ya uboreshaji wa daftari yatahusisha maeneo makuu matano ambayo ni uandikishaji wapigakura wapya wenye miaka 18 au zaidi au watakaotimiza umri huo kabla au siku ya uchaguzi mwaka 2025, kutoa fursa kwa wapigakura kuhamisha taarifa zao ambao wamehama kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda jingine na kutoa fursa wanaoboresha taarifa zao, kama jina, kutoa kadi kwa wapiga kura waliopoteza au ambao kadi zao zimeharibika na kuondoa wapiga kura waliopoteza sifa.

Kwenye majaribio hayo tume itajaribu mfumo wa uandikishaji wa wapiga kura ulioboreshwa unaoitwa Online Voters Registration System (OVRS) utakaomwezesha mpigakura aliyemo kwenye daftari kuanzisha mchakato wa awali wa kuboresha taarifa zake , kuzibadilisha au kuhama kata au jimbo kwa njia ya mtandao kwa kutumia simu ya mkononi au kompyuta, anasema Kailima.

Mkurugunzi wa Uchaguzi anasisitiza kuwa ushirikiano kutoka kwa wadau wa uboreshaji wa daftari ni pamoja na vyama vya siasa, viongozi wa dini, vyombo vya habari, wazee wa kimila, wazee maarufu, asasi za kiraia, wawakilishi wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ni muhimu kufanikisha zoezi hilo la uboreshaji wa majaribio.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wakitoa maoni yao kuhusu zoezi hilo wadau wa uchaguzi wanapongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa uamuzi wake wa kuendelea kutekeleza majukumu kwa uwazi na kuendeleza utamaduni wa kuwashirikisha wadau wa uchaguzi.

Vyama vya siasa aidha viliishukuru tume kwa kuruhusu vishiriki kwenye zoezi hilo kwa kuweka wakala mmoja katika kila kituo cha kuandikisha wapigakura ili waweze kushuhudia na kujiridhisha juu ya taratibu zitakazotumika wakati wa majaribio ya uboreshaji wa daftari.

## RAIS GEORGE WEAH WA LIBERIA

# Japo ameshindwa jina lake linavuma, amekubali kubwagwa, sifa kila kona

• Taifa 'linatisha' uchaguzi huru na haki unaoaminika, aliyeshinda kasahaulika

**Na Gaudensia Mngumi**

GEORGE Weah, Rais wa Liberia aliyeshindwa uchaguzi wiki iliyopita na kuondolewa ikulu na mpinzani wake anasifika kwa kupenda amani na haki.

Mwanasoka huyu mahiri, alishika wadhifa huo mkubwa katika taifa lake, kuanzia 2018, akiingia ikulu ya Liberia, baada ya kuwa mchezaji nguli wa Afrika aliyetwaa tuzo ya Ballon d'Or mwaka 1995.

Ni baada ya kuwashinda wakali Jurgen Klinsmann wa Ujerumani na Jari Litmanen wa Ajax kwenye taji hilo la kifahari,linalotolewa na Ufaransa.

Akiwa na miaka 57, anaondolewa ikulu na mpinzani wake Mwanasiasa mkongwe Joseph Boakai (78). Anamrudisha nyumbani Weah na jana akatangazwa kuwa mshindi wa uchaguzi wa urais wa Liberia 2023.

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) Davidetta Lansanah, anawaambia wanahabari kuwa Boakai ameshinda kwa asilimia 50.64 ya kura dhidi ya asilimia 49.36 ya kura alizopata mbobezi wa zamani wa soka duniani, George Weah, kwa mujibu wa DW.

Rais huyo mteule amemshinda mpinzani wake kwa tofauti ya kura 20,567 pekee lakini Weah alikuwa tayari amekubali kushindwa kuanzia Ijumaa iliyopita, kutokana na zaidi ya asilimia 99 ya matokeo vituoni kuonyesha kuwa mpinzani wake alikuwa amemwacha mbali.



Rais mteule Joe Boakai wanayemwita 'cha usingizi'



George Weah, aliyebwagwa wiki iliyopita. **PICHA ZOTE MTANDAO**

### SIFA KEMKEM

George Weah ambaye ni mshindi wa tuzo ya mchezaji bora duniani ya Ballon d'or mwaka 1995, amepata sifa kimataifa kwa kukubali kushindwa na kukabidhi madaraka bila ya vurugu, akiamsha salamu za pongezi kutoka kwa viongozi mbalimbali maarufu duniani akiwamo Joe Biden.

Marekani inatuma pongezi kwa Boakai huku akimsifu George Weah kwa kuheshimu chaguo la watu na kwa kuonyesha uzalendo na ukomavu wa kisiasa, inasema DW.

Msaidizi maalum wa Weah, Sekou Kalasco Jomanday, anasema hatua yake kukubali kushindwa haikushangaza akiongeza:"Huyo ni mtu wa aina yake, ni mpenda amani ambaye anaamini mapenzi ya watu yanapaswa kuheshimiwa kila wakati na ataendelea kufanya hivyo," anaiambia BBC.

Weah anasifika kwa kuangalia takwimu na kugundua njia yake ya ushindi ilikuwa finyu au haiwezekani tena, anakubali yaishe.

Huo ukilezwa kuwa ni ushindi kwa demokrasia ya Liberia. Kwa vile aliye madarakani kakubali kuwa ameshindwa ni uthibitisho wa ukomavu wa demokrasia ya taifa hilo, inaongeza BBC.

Uchaguzi huo ni wa kwanza tangu kuondoka kwa walinda amani wa Umoja wa Mataifa ambao walitumwa baada ya kumalizika rasmi kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe mwaka 2003.

Rais haamini kwamba mtu mmoja anapaswa kupoteza maisha kwa sababu ya mapambano yoyote ya kisiasa au nia ya mtu mmoja kuwa rais wa nchi, inaongeza.

Samora Wolokollie, Naibu Waziri wa Fedha wa Liberia naye anamshangilia akiambia BBC kuwa rais alikuwa amedhamiria kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa "uadilifu mkubwa, uwazi , ukweli na uaminifu wa hali ya juu".

"Atakumbukwa milele kwa hatua hii ya kizalendo." Jumuiya ya Kanda ya Uchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS), pia imetoa taarifa ya kumshukuru Weah kwa kuwa mzalendo na mpenda amani.

"Kukubali kwako kwa neema matokeo ya uchaguzi ni dalili ya uzalendo wako na kujitolea kwako katika kuimarisha amani na usalama Liberia," anasema Omar Alieu Touray, Rais wa Tume ya ECOWAS, ambaye pia anapongeza uchaguzi huru, wa haki na ulioandaliwa kwa uhuru na umahiri, inaripoti BBC..

ECOWAS imekuwa mstari wa mbele katika kuleta utulivu nchini Liberia , tena ikipeleka wanajeshi 12,000 nchini humo katika miaka ya 1990, huku wanajeshi wa Nigeria wakiwa uti wa mgongo wa kikosi cha Umoja wa Kujilinda wa Nchi za Afrika Magharibi ECOMOG.

### KAWAIDA KIUKANDA

Jina la George Weah linavuma kwenye mitandao ya kijamii kote Afrika, na Nigeria ambako watu wamesema ingawa kupongezwa kwake ni hatua nzuri, lakini sio wa kwanza.

"Ni matokeo ya 'Jonathan' rais wa zamani wa Nigeria, Goodluck Jonathan, alitaka muhula mwingine 2015, akashindwa na mpinzani wake Muhammadu Buhari, akamwita na kumpongeza," anakumbusha Mhariri Mkuu wa zamani wa gazeti la Daily Trust la Nigeria.

"Haijawahi kushuhudiwa kwa sababu kwa kawaida marais walioko madaraka hawatakubali kuondolewa ndiyo maana Weah pia ameonyesha neema kubwa kwa kukubali matakwa ya Waliberia na kumpongeza mpinzani wake,"anaongeza na kwamba ni fahari kwa Nigeria kwamba Liberia inafuata nyayo zake.

### JOSEPH BOAKAI

Ndiye rais mteule. Ni mpinzani wa Weah , ambaye amekuwa Makamu wa Rais kwa miaka 12 chini ya Rais Ellen Johnson Sirleaf, rais wa kwanza mwanamke Mwafrika aliyechaguliwa.

Rais mpya ataanza rasmi kazi Januari 2024 atakapoapishwa. Kiongozi huyu alijitambulisha kama "gari la kasi lililoegeshwa gereji", maneno aliyoyatumia kwenye kampeni mwaka 2017, aliposhindwa na Weah.

Hii ni safari ya pili kuchuana naye. Licha ya wapinzani na watani wake kumuita cha usingizi "Sleepy Joe" baada ya ripoti kuonyesha kuwa anasinzia kwenye hafla na matukio mengi rasmi.

Safari hii Boakai ameahidi kurejesha matumaini nchini Liberia na kuzuia nchi hiyo kuangukia kwenye maporomoko ya mwamba (cliff), inaandika BBC.

### YAKUJIVUNIA

Tovuti yake inaorodhesha mafanikio 58 katika uongozi wake akitaja , kutetea vyuo vya jamii hadi kupatanisha mizozo mbalimbali kote Liberia na kuwa na amani ya kudumu.

Mafanikio makubwa zaidi kutoka wakati wake madarakani, hata hivyo, yalikuwa ni kuleta amani na utulivu kila mahali kufuta maasi yaliyoitawala nchi hiyo karibu miaka 15 ya vita.

Marais wa Liberia waliohusika na vita Desemba 1989 ni pamoja na Samuel Doe na Charles Taylor, amba baada ya kuondoka madaraka Rais Ellen Sirleaf aliongoza taifa hilo kwa amani kuanzia 2006 hadi 2018.

## UWT INA NDOTO KUUNGANISHA WANAWAKE BILA KUJALI ITIKADI KUMCHAGUE RAIS SAMIA 2025

**INATOKA UK. 11**

nao waungane nasi kumrudisha Rais Samia. Wanawake ni jeshi kubwa, ninaamini kwamba mwaka 2025 ndio ambao wanaume watajua hilo. Tumeamua kuunganisha nguvu, hatuwezi kutenganishwa na vyama tunapokuwa na jambo letu kama wanawake, hivyo

**SWALI:** Penye mafanikio huwa hapakosi changamoto, ni changamoto gani unazokutana nazo kwenye kampeni hiyo?

**JIBU:** N kweli kwenye mafanikio hapakosi changamoto, lakini nikuhakikishie kuwa sijakutana na changamoto, hasa kwa kuzingatia kwamba sisi wanawake wote wa Tanzania ajenda yetu ni moja ya kumnyanyua mwanamke, na tumeamua kumnyanyua Rais Samia aongoze tena miaka mitano ijayo.

Hivyo tunakwenda vizuri katika hili, Rais Samia amefanya makubwa kwa ajili ya Watanzania, lakini pia akiwapa kipaumbele wanawake katika uongozi, kujenga sekondari za wasichana kila mkoa, na mengine mengi, ninaamini hakuna mwanamke anayepingana na hilo hata atoke chama cha upinzani.

**SWALI:** Umepanga kutumia muda kampeni hiyo ya kuunganisha wanawake kuzungumza lugha moja kuhusu Rais Samia kwenye uchaguzi mkuu ujao?

**JIBU:** Nimeeleza awali kuwa mwisho wa uchaguzi ndio mwanzo wa mwingine. Maana yangu ni kwamba kampeni hii ni endelevu hadi wakati wa uchaguzi. Nitaendelea kushirikiana na wenzangu kuwahamasisha ili kuhakikisha lengo letu linatumia la kumweka Rais Samia madarakani amalizie muda wake.



## CCWT kuanza uchaguzi, yaonya wala rushwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME Huru ya Uchaguzi ya Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT) imetangaza kuanza rasmi kwa mchakato wa uchaguzi ngazi ya kijiji hadi taifa huku ikionya wagombea kutojihusisha na vitendo vya rushwa.

Ilisema wakibaini mgombea yeyote kujihusisha na vitendo vya rushwa ataondolewa mara moja kwenye kinyang'anyiro hicho.

Akitoa taarifa hiyo kwa waandishi wa habari juzi, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Charles Malagwa, alisema uchaguzi ngazi ya vijiji na kata ulianza Novemba 20 hadi Desemba 10, 2023, mwaka huu.

Malagwa, alisema rushwa ni moja ya sababu ambayo imekitesa sana chama hicho hivyo katika uchaguzi huo tume imejipanga kukomesha vitendo hivyo.

Alisema wameipanga tume kuhakikisha hakuna nafasi kwa wagombea kutoa rushwa ili wachaguliwe na kuwasihi wanachama wote wajitokeze ili kupata viongozi waadilifu watakao kiongoza chama hicho.

Aidha, alisema chama hicho kinahitaji viongozi thabiti watakaosaidia kutatua kero za wafugaji ikiwamo migogoro na wakulima malisho, majosho na maji inayoendelea.

Aidha, alisema ni matumaini ya tume kuwa viongozi watakaopatikana wataendeleza jitihada ambazo zimefanywa na chama hicho na serikali za kutatua kero za wafugaji nchini ili kuongeza tija kwenye sekta ya mifugo nchini.

"Tume imeketi leo, pamoja na mambo mengine imepokea hadidu za rejea kutoka kamati tendaji, kwa mujibu ya ibara ya 2 ya sehemu ya 4 ya katiba ya chama cha wafugaji ya mwaka 2013, toleo la Machi 2023, tume imepewa mamlaka ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za uchaguzi wa chama cha wafugaji Tanzania," alisema.

Aidha, alisema uchaguzi ngazi ya wilaya kuchukua na kurudisha fomu ni kuanzia Novemba 25 hadi 30, 2023, na kujadili wagombea ni Desemba 1 hadi 4 ambapo uchaguzi utakuwa ni Desemba 5 hadi 10, 2023.

Kadhalika, alisema uchaguzi ngazi ya kanda kuchukua fomu na kurudisha ni kuanzia Desemba 20 hadi 27, 2023, kujadili wagombea ni Desemba 28 hadi 31 na uchaguzi utafanyika Januari 4, 2024.

Vile vile, alisema uchaguzi ngazi ya taifa kuchukua fomu ni kuanzia Desemba 20 hadi 27, 2023 kujadili wagombea ni Jauari 6 hadi 7, 2024 na uchaguzi utakuwa ni Januari 8, 2024.

Hata hivyo, alisema maelekezo mengine yataendelea kutolewa na tume kulingana mwenendo wa mchakato huo wa uchaguzi utakavyokuwa unaendelea.

# Sheria mpya PPRA kuboresha ununuzi wa umma nchini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

OFISA Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Eliakim Maswi, amesema kutungwa kwa sheria mpya ya ununuzi wa umma itasaidia kuboresha sekta ya ununuzi wa umma nchini.

Akizungumza na Nipashe Maswi alisema, maboresho yaliyofanywa kwenye sheria hiyo inayotarajiwa kuanza kutumika hivi karibuni yanalenga kuleta uwazi, uwajibikaji na thamani ya fedha inapatikana katika michakato ya ununuzi.

"Serikali ya awamu ya sita imekuwa sikivu, maisha ya Mtanzania katika ununuzi wa Umma sasa yanabadilika, kilio cha muda mrefu cha rushwa na ukiukwaji wa sheria katika ununuzi wa umma sasa kimepatiwa ufumbuzi," alisema.

Alitaja mafanikio yanatarajiwa katika sheria hiyo kuwa ni kujenga mazingira rafiki kwa wazabuni wazawa kwa kuwawekea upendeleo wa kushinda zabuni katika zabuni zenye ushindani wa kimataifa.

Alisema sheria hiyo pia imeweka vigezo vya jumla kwa makandarasi au washauri elekezi kupata upendeleo wa zabuni za kitaifa katika kampuni binafsi au ushirika wa kampuni za ndani.

Alitaja baadhi ya vigezo hivyo kuwa ni kampuni hizo ziwe zimeanzishwa au kusajiliwa ndani ya Tanzania na sehemu kubwa ya mtaji wa hisa zilizolipwa za kampuni binafsi iwe inamilikiwa na raia wa Tanzania.

Kigezo kingine kwa mujibu wa Maswa ni kampuni hizo zisiwe na utaratibu unaoelekeza sehemu kubwa ya faida halisi kutolewa au kulipwa kwa watu ambao si raia wa Tanzania au kwa kampuni ambazo zisingekuwa na sifa chini ya kifungu husika.

Kigezo kingine ni eneo la matumizi ya wataalamu wa ndani katika mikataba ya kazi za ujenzi na huduma zisizo za kitaalamu, upendeleo kwa bidhaa za ndani, uingiaji wa ushirika au mikataba midogo na kampuni za ndani pamoja na upendeleo wa utoaji zabuni kwa makundi maalum ya kijamii.

Alisema maboresho ya sheria hiyo yanaenda sambamba na ujenzi wa mfumo mpya wa ununuzi wa umma kielektroniki (NeST) unaoendelea kuongeza ufanisi katika sekta ya ununuzi nchini tangu ulipoanza kutumika miezi michache iliyopita mwaka huu.




Msemaji Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO), Mobhare Matinyi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana kuhusu mwendelezo wa ziara zake mikoani. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# MSD yakabidhi vifaa tiba vya mil. 222/- Ikungi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

BOHARI ya Dawa (MSD) imekabidhi vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya Sh.milioni 222.47 katika hospitali za wilaya na vituo vya afya zilizopo katika za Wilaya za Ikungi na Singida.

Meneja wa MSD Kanda ya Dodoma, Mwanashehe Jumaa, akizungumza baada ya kukabidhi vifaa hivyo kwa viongozi wa wilaya hizo, alisema vitasaidia kuboresha huduma ya uzazi katika wilaya hiyo.

Alitaja vifaa hivyo kuwa ni pamoja na majenereta, vifaa vitakavyotumika kuhudumia watoto wanaozaliwa kabla ya muda, kitanda cha kufanyia upasuaji, Ultra-Sound.

"Kazi yetu kubwa sisi MSD ni kununua, kuzalisha, kuhifadhi na kusambaza bidhaa za afya na vitendanishi hapa nchini ambayo tunaifanya kwa mamlaka ya kisheria," alisema.

Jumaa alisema katika wilaya hiyo MSD ilikuwa inakamilisha vifaa vilivyosalia kutoka kwenye fedha iliyopokea zaidi ya Sh. milioni 300 ili kukamilisha usambazaji wake.

Jumaa alisema pia MSD ilipokea zaidi ya Sh. milioni 700 ambapo pia kuna vifaa vya zaidi ya Sh.milioni 72 ambavyo vimekabidhiwa kwa ajili ya kuendelea kuboresha huduma za afya.

"Ukiangalia muda tuliopokea fedha hizi na utekelezaji wa kupeleka vifaa hivyo ni muda mfupi sana na hiyo imetokana na Serikali kuboresha huduma za MSD na kufikia hatua hii," alisema.

Alisema serikali imekuwa ikitoa fedha na MSD ikinunua na kusambaza vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya kote nchini jambo linalojenga morali kwa watumishi wa sekta ya afya kuipenda kazi wanayoifanya.

Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, aliishukuru serikali kwa kupelekwa kwa vifaa hivyo kwa kuwa vitasaidia wananchi kupata huduma za uhakika za matibabu.

Mbunge wa Singida Kaskazini, Ramadhani Ighondo, alisema kupelekwa kwa jenereta na gari la kubebea wagonjwa kusaidia kuokoa maisha ya wajawazito ambao wengi wao walikuwa wakipoteza maisha kwa kukosa umeme wakati wa upasuaji.





# TANAPA, WWF kuwapa tuzo wanaohifadhi mazingira

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), kupitia Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kushirikiana na Shirika la Uhifadhi wa Maliasili la WWF, limeanzisha tuzo maalumu ya kutunza mazingira itakayotolewa kwa wananchi watakaohifadhi vizuri vyanzo vya maji.

Wananchi wanaolengwa kushiriki kwenye kinyang'anyiro cha tuzo hiyo ni wale watakaotunza vizuri vyanzo vya maji vya Mto Ruaha ambao ni muhimu kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwamo kilimo, uzalishaji wa umeme na shughuli za uvuvi.

Mwakilishi wa Shirika la WWF, Dk. Abubakary Kijoji, aliyasema hayo kwenye kikao cha wadau wa mazingira kilichofanyika jijini Mbeya na kushirikisha wadau kutoka katika mikoa mitatu ya Mbeya, Iringa na Njombe.

Alisema wanakusudia kuunda chombo maalumu ambacho kitakuwa kinasimamia tuzo hizo kitakachokuwa na wajumbe kutoka katika sekta binafsi na sekta ya umma.

"Tutazishirikisha pia serikali za mikoa na wilaya zote ambazo zipo kwenye eneo hili, pia wadau wa maendeleo tutawashirikisha ili kuhakikisha tunakuwa na chombo ambacho ni imara na kitatuletea matokeo chanya," alisema Dk. Kijoji.

Akizungumza kwa niaba ya serikali ya Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Denis Mwila, alisema tuzo hiyo itakuwa na faida kubwa kwa wananchi, serikali pamoja na wadau mbalimbali wa mazingira.

Alisema tuzo hiyo itasaidia kuhamasisha wananchi kutunza maji ambayo yanatumika kwenye shughuli mbalimbali ikiwamo matumizi ya nyumbani, kutunza viumbe hai wanaoishi kwenye maji, pamoja na uzalishaji wa nishati ya umeme.

"Tuzo hii itasaidia wananchi kutunza mazingira kwa ajili ya kulinda ikolojia kwenye maeneo yetu, lakini watapata faida kwa kupata tuzo hiyo, vilevile maji watakayotunza watayatumia hata wao wenyewe kwenye shughuli mbalimbali," alisema Kanali Mwila.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wanging'ombe mkoani Njombe, Mariam Muhaji, alisema tuzo hiyo itawahamasisha wananchi katika maeneo mbalimbali kushiriki kutunza mazingira kwenye maeneo yao.

Alisema watashiriki pia kwenye kuchangia mfuko wa tuzo hizo kutokana na mapato ya ndani ili kuufanya mfuko huo kuwa endelevu na kutoa huduma kwa muda mrefu.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbarali, Misana Kwangula, alisema wakati wa kuandaa bajeti ya halmashauri watatenga fedha kwa ajili ya mazingira ambazo zitapelekwa kwenye mfuko wa tuzo.

Mikoa ya Mbeya, Njombe na Iringa ni maeneo ambayo ndiyo yana vyanzo vingi vya maji ambayo ni muhimu kwa ajili ya ikolojia ya Mto Ruaha Mkuu na maeneo ambayo yamekuwa yakikabiliwa na tatizo kubwa la uharibifu wa mazingira.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (katikati), akiwa na baadhi ya viongozi akikagua ujenzi wa barabara ya Ndudilo-Itete, inayojengwa kwa kiwango cha lami wilayani Rungwe, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Waomba kuharakishwa mchakato kufundishwa Kiswahili shuleni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa lugha ya Kiswahili wameiomba serikali kuharakisha mchakato wa kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia kuanzia shule za msingi mpaka vyuo vikuu ili kupanua wigo wa wanafunzi kupata maarifa zaidi.

Wadau wa Kiswahili mkoani Mbeya walitoa ombi hilo wakati wa uzinduzi wa vitabu viwili vya kufundishia lugha ya Kiswahili vya Mwalimu Daud Mulungu ambaye ni miongoni mwa waandishi wachanga wa vitabu wanaodaiwa kuwa na weledi kwenye matumizi ya Kiswahili.

Mmoja wa wadau hao, Mwalimu Simon Komba, alisema matumizi ya lugha ya Kiswahili yatasaidia kueneza vizuri utamaduni wa Mtanzania kwenye mataifa mengine.

Alisema Tanzania ikianzisha utaratibu huo na ikatunga sera imara itakuwa mfano kwa mataifa mengine ya Afrika Mashariki na duniani na kwamba itakuwa rahisi zaidi wanafunzi kuelewa kile wanachofundishwa.

"Kiswahili ni sehemu ya utamaduni wetu, kwa hiyo nashauri serikali ianzishe misingi bora na imara ya matumizi ya lugha hii kwenye kufundishia, sera ziwekwe vizuri ili lugha hii rasmi ianze kutumika," alisema Komba.

Naye Agustino Sikanda alisema kuna baadhi ya wanafunzi huwa wanashindwa kuelewa vizuri wanachofundishwa kwa sababu ya lugha inayotumika hasa wanafunzi wanapoanza elimu ya sekondari.

Alisema wanafunzi wengi wanajifunza kwa lugha ya Kiswahili wanapokuwa shule ya msingi lakini wanapoanza sekondari wanakutana na Kiingereza ambacho kinatumika kama lugha ya kufundishia hali ambayo inasababisha ugumu wa kuelewa.

Akizungumzia uzinduzi wa vitabu hivyo Mkurugenzi wa Lugha Mwandamizi kutoka Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Mussa Kaoneka, alimpongeza Mwalimu Mulungu kwa ubunifu alioutumia kwenye uandaaji wa vitabu hivyo.

Alisema BAKITA itahakikisha inavipatia ithibati vitabu hivyo ili vianze kutumika kufundishia kwenye shule za sekondari nchini.

# Waiangukia serikali ya kijiji kudhibiti moto shambani

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI wa Kijiji cha Kifanya, Halmashauri ya Mji wa Njombe, mkoani Njombe, wameiomba serikali ya kijiji hicho kuchukua hatua za haraka kukabiliana na majanga ya moto yanayounguza maelfu ya mashamba ya miti hususani katika kipindi cha maandalizi ya mashamba.

Wakizungumza katika mkutano wa kijiji hicho, wananchi hao walisema kwamba wanaunguliwa mashamba ya miti na ushiriki wa wananchi kuzima moto umekuwa mdogo tofauti na kipindi kilichopita.

"Hivi sasa wananchi wanaunguliwa maelfu ya mashamba ya miti na ushiriki wa kuzima moto umekuwa ni mdogo tofauti na kipindi kilichopita," alisema Kasian Lwiva.

Naye Bushery Kilasi alisema kuna baadhi ya watu wanachoma moto huo kwa makusudi kwa sababu mbalimbali na wapo waliokamatwa lakini wakaachiwa bila kuchukuliwa hatua zozote.

"Hivi ni vita baridi na itakuwa ya moto zaidi, mtu anachoma makusudi na hana shida na ikitokea amekamatwa anayetorosha moto kesi inaishia ofisini mambo yameisha," anasema Kilasi.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kifanya, Halmashauri ya Mji Njombe, Bariki Kabelege alisema kuwa wamekubaliana kutoa Sh.20,000 mtu yeyote atakayebaini kuwapo kwa moto katika eneo lolote hata kama haujaanza kuleta madhara na kwa atakayesababisha atapingwa faini ya Sh. 50,000.

"Kwa sababu kasi ya mashamba kuungua ni kubwa kwetu sisi, moto unaanza wakati wa kuandaa mashamba kama vinyungu hasa hasa kuanzia mwezi wa saba mpaka leo ninavyosema ni hekta nyingi, lakini ni hekta zaidi ya 200 zimeteketea ambazo zilikuwa na mazao kitu ambacho kinarudisha nyuma," alisema Kabelege.

Diwani wa Kata ya Kifanya, Nolasko Mtewele, alisema pamoja na kuwapo kwa sheria ndogo ndogo zinazoeleza hatua za kukabiliana na moto lakini bado zimekuwa hazifanyi kazi vyema.

"Naomba vijiji vyote vinavyozunguka Kata ya Kifanya vihakikishe kwenye suala la moto vinaweka kipaumbele sana, kwa sababu uchumi wetu kwenye kata hii tunaonekana tupo vizuri kwa sababu ya misitu ambayo tunapata mbao kwa asilimia kubwa tunapata faida," alisema Mtewele.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kifanya, Alberto Mkalawa, alisema wameweka sheria ndogo za kijiji kwamba ambazo zinaelekeza kuwa yeyote anayehitaji kuchoma shamba kuanzia eka moja uwe na watu wasiopungua 10.

"Tukaja tukagundua changamoto wale watu wakishapata watu 10 anabeba na pombe anaenda nayo huko shambani madhara yake watakunywa ile pombe hawatakuwa makini kuzingatia ule moto namna walivyochoma lile shamba wanatekelezea siku ya pili na bahati mbaya ikitokea wanashindwa kudhibiti," alisema Mkalawa.



## Rais Samia apongezwa uwekezaji sekta ya mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi imempongeza, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mzuri katika sekta ya mawasiliano kupitia mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) unayoiwezesha mamlaka hiyo kusimamia huduma na usalama wa mawasiliano nchini.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Rashid Abdallah, alitoa pongezi hizo jana baada ya kupokea wasilisho la taarifa maalum ya mamlaka hiyo katika ukumbi wa TCRA, Dar es Salam.

Alisema kamati hiyo inaridhishwa na kazi nzuri inayofanywa na mamlaka hiyo hasa katika nyanja ya utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Wakitoa michango yao wajumbe wa kamati hiyo wameishauri Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kukiongezea nguvu kitengo cha kusimamia uhalifu wa mitandaoni ili kitekeleza majukumu yake kwa ustadi.

Aidha, wajumbe hao wameishauri mamlaka ya mawasiliano kuendelea kudhibiti changamoto za mitandaoni ikiwamo utapeli pamoja na changamoto ya mmong'onyoko wa maadili kwa vijana.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Jabiri Kuwe Bakari, alisema mamlaka hiyo inaendelea kusimamia majukumu yake kwa uweledi ili kufikia lengo la kutoa huduma bora kwa Watanzania.

Alisema Tanzania inaendelea kufanya vizuri katika utoaji wa huduma za mawasiliano ikiwamo huduma za miamala ya kifedha kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Ziara ya wajumbe wa kamati ya mawasiliano, ardhi na nishati inalenga kujifunza pamoja na kubadilishana uzoefu.

# Matukio ukatili wa kijinsia yaongezeka Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MATUKIO ya ukatili na udhalilishaji yameongezeka kwa asilimia 28 kwa kipindi cha mwezi mmoja kutoka matukio 157 yaliyoripotiwa Septemba hadi 199 Oktoba, mwaka huu.

Akitoa takwimu hizo jana visiwani humo, Mtakwimu kutoka Divisheni ya Jinsia na Ajira katika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, Ramla Hassana Pandu alisema katika idadi ya matukio ya mwezi Oktoba waathirika wengi ni watoto kwa asilimia 78.9, wanawake 16.1 na wanaume asilimia 5.0.

Alisema matukio ya kubaka kwa mwezi wa Septemba yalikuwa 59 ambapo kwa mwezi wa Oktoba yamefikia 89, ikiwa ni ongezeka la makosa 30, kulawiti na kunajisi yalikuwa 15, mwezi Oktoba yamefikia 22, makosa ya kuingilia kinyume na maumbile Septemba yalikuwa sita na Oktoba ni 13, kutorosha Septemba makosa 11 na Oktoba makosa 10.

Aidha makosa ya shambulio la aibu au kukashifu kwa mwezi yalikuwa 24 na Oktoba yamefikia 22, makosa ya shambulio kwa mwezi wa Septemba yalikuwa 42 ila kwa mwezi wa Oktoba yameongezeka na kufikia 43.


Akizitaja wilaya zinazoongoza kwa matukio ya ukatili na udhalilishaji kuwa ni Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja zimeripotiwa kuwa na matukio mengi zikilinganishwa na wilaya zingine kwa matukio 52 sawa na asilimia 26.1 kwa kila wilaya.

Kwa mujibu wa mtakwimu huyo, eneo linalofuatia ni Wilaya ya Magharibi A' yenye matukio 37 sawa na asilimia 18.6 huku Wilaya za Micheweni na Mkoani ikiwa na idadi ndogo ya matukio ya udhalilishaji kwa kuwa na matukio matatu sawa na asilimia 1.5 kwa kila wilaya.

Ramla alisema Wilaya ya Mjini imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio ya kubaka ikilinganishwa na wilaya nyingine kwa matukio 22 sawa na asilimia 24.7 kati ya matukio yote ya kubaka yaliyoripotiwa, ikifuatiwa na Wilaya ya Magharibi B kwa matukio ya ubakaji 19 sawa na asilimia 21.3.

Kati ya matukio 89 ya ubakaji yaliyoripotiwa kwa mwezi wa Oktoba 2023, matukio 15 sawa na asilimia 16.9 yameripotiwa kwa wanawake na matukio 74 yameripotiwa kwa wasichana sawa na asilimia 83.1.

Akitaja hatua zilizochukuliwa alisema kuwa kati ya matukio yote 199, matukio 139 yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 69.9, matukio 57 sawa na asilimia 28.6 yapo Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na matukio matatu 3 sawa na asilimia 1.5 yapo mahakamani.




Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhammed Mussa (katikati), akikabidhi cheti cha utambulisho kwa Mwenyekiti wa Baraza la Nane la Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Hamida Ahmad Muhammed (kushoto), baada ya uzinduzi wa baraza hilo, visiwani Zanzibar juzi. Kulia ni Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Mohammed Makame Haji. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Uhusiano Zanzibar, India waendelea kuimarika

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema uhusiano mzuri uliopo baina ya Zanzibar na India umeendelea kuimarika hali inayochangia kuleta maendeleo katika nchi hizo.

Alisema, mbali na ushirikiano wa karibu uliopo baina ya serikali za pande mbili hizo pia uhusiano kati ya Wahindi na Watanzania ni wa muda mrefu na diaspora wengi raia wa India wapo nchini kwa miaka mingi wakiwa na shughuli mbalimbali za jamii na uchumi.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu, Zanzibar alipomkaribisha kwa mara ya kwanza Zanzibar, Waziri wa Nchi na Mambo ya Nje wa India, Shri V. Muraeedharan.

Rais Dk. Mwinyi alisema India imekua ikiunga mkono Tanzania husussan Zanzibar kwenye masuala mbalimbali ya maendeleo ikiwamo sekta ya maji na elimu kwa kutoa fursa nyingi za udhamini wa masomo nchini India kwa Watanzania wengi.

Aidha, Dk. Mwinyi alisema uamuzi wa India kuanzisha tawi la Chuo cha IIT Madrasa kwa Zanzibar ni mafanikio makubwa ya ushirikiano uliopo baina ya nchi hizo na ni fursa azimu ya kuiweka Zanzibar kwenye ramani ya ulimwengu huku kukiwa na matumaini yakupokea wageni wengi kutoka nje ya Tanzania kuja kujiunga na chuo hicho.

Rais Dk. Mwinyi aliishukuru serikali ya India kwa kuiunga mkono Tanzania na kushauri kuongezwa vitivo zaidi katika chuo hicho ili kuchochea wanafunzi wengi kujiunga.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Waziri wa Nchi na Mambo ya Nje anayeshughulikia pia masuala ya Bunge nchini India, Shri Muraeedharan, alisema uhusiano baina ya India na Zanzibar ulianza kabla ya Tanganyika na Zanzibar kuungana, historia iliyoziunganisha pande mbili hizo kiuchumi na jamii.

Alisema uwapo wa Chuo cha IIT Madrasa Zanzibar, waziri alisema ni njia mojawapo ya kudumisha dipomasia iliopo baina ya Tanzania husussan Zanzibar na India sambamba na kuzalisha viongozi wengi wenye fani na teknolojia ya hali ya juu kutoka kampasi ya Zanzibar.

Katika ziara yake, Zanzibar, Waziri Muraeedharan alipata fursa ya kutembelea Chuo cha IIT Madrasa kilichoko Bweleo, Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja pamoja na kuangalia eneo litakalojengwa Chuo cha IIT Madrasa, Kampasi ya Zanzibar Fumba.

Hafla hiyo pia, ilihudhuriwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar, Mwanahamisi Ameir, Balozi wa India nchini Tanzania Binaya Pradhan na Balozi Mdogo wa India aliyepo Zanzibar, Dk. Kumar Praveen.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALHAMDU JUMANNE MASUDI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 627 DRN – TOYOTA WISH.** Chassis namba **ZNE100136527.** Engina namba **1ZZ1762217.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/6758/2023.**

## KUPOTEA KWA HATI YA SHAMBA

**ISRAEL ZAKAYO SEKIRASA** anatangaza kupotelewa na hati ya shamba lenye kitalu namba 3714 lililopo MADALE , KINONDONI DAR ES SALAAM.Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na ISRAEL ZAKAYO SEKIRASA kwa simu namba 0757299606.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/42661/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSENO.147 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late JOYCE EZEKIEL MUTOKA of Maili Mbili within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY ONESMO AMOS RUGAKINGILA**

**GENERAL CITATION**
**( Rule 75 of Probate Rules Gn.369 of 163)**

ALLPERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are here by cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above-named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 22 Day of 11, 2023

Date at Dodoma this 30 Day of OCTOBER, 2023.

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Bukoba Mjini,Mkoa wa Kagera**
**Shauri la Madai Na 367/2023**
**Jina la Mdai Mwajabu Khalid**
**Jina la Mdaiwa Avitus Mujuni**
**KUITWA SHAURINI**

**Kwa Avitus Mujuni**

Kwa kuwa mdai ameleta madai ya Tsh 10,654,000 Milioni kumi laki sita na elfu hamsini na nne.Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 30 Mwezi 11 Mwaka 2023 saa 3.00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo.Na kwa kuwa ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi walio na vielelelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO.Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini.Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 09 Mwezi 11 Mwaka 2023

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya BUGANDO Wilaya ya GEITA**
**Mkoa ............GEITA**
**Shauri la TALAKA Na 92/2023**
**Jina la Mdai: EMMANUEL MADARAKA**
**Jina la Mdaiwa: STEPHANIA ERASTO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuniya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:STEPHANIA ERASTO WA LWEZELA**

AMRI: - Unaamriwa na Jamuhuri uhudhurie Mahakamani hapa siku ya Jumanne tarehe 22/11/2023 saa 2:00 Asubuhi ili ujibu madai ya Fedha Tsh.3,300,000/-. Usipohudhuria kesi itasikilizwa bila wewe kuwepo

Unaonywa usikose kuhudhuria.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 16 Mwezi 11 Mwaka 2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
BUGANDO

## NAFASI ZA KAZI

Ualimu Masomo ya **Hesabu, Science, Kiswahili na Kiingereza.**

Pia wanatakiwa walimu Wastaafu isizidi miaka mitatu (3) iliyopita kwa ajili ya ukaguzi.

**SIMU: 0783 298 900**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NICHOLAUSI GEREVAS NDENZAKO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 703 ADZ aina ya Toyota Hilux, ChassisNo.YN800001943, EngineNo.2Y0565239. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/9136/2023.**

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 1759/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SALUM ALTO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA NYAMKA SALUM LWAMBANO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 22 mwezi 12 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetokewa leo tarehe 21 mwezi 11 mwaka 2023.

HAKIMU

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 146 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late GODFREY DANIEL KAULA of Khungu within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY DANIEL KAULA AND MARIAM HASSAN**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 of 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are here by cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above-named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 22 Day of 11,2023

Date at Dodoma this 30 Day of OCTOBER,2023.

RESIDENT MAGISTRATE

**FOMU MADAI – 12**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MADAI 19/2023**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MUHEZA**
**Kituo cha NGOMENI Mkoa TANGA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 19, 2023**
**Jina la mdai: MOHAMED OMARY**
**Jina la mdaiwa: OMARY MIRAMBO**
**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(Kanuni ya 62 ya Kanuni za uendeshaji mashauri Mahakama za Mwanzo)**
**KWA: OMARY MIRAMBO**

KWAMBA Mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe 23 Mwezi wa 11 Mwaka 2023 kueleza kwanini Hukumu isitekelezwe dhidi yako.

Hati hii Imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 20/11/2023.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
NGOMENI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MUFINDI**
**Kituo cha MAFINGA**
**Mkoa IRINGA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na...40/2023**
**Jina la mdai MUCOBA BANK PLC**
**Jina la Mdaiwa TUJISHUGHULISHE KINAMAMA GROUP**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za mwanzo)**

**Kwa TUJISHUGHULISHE KINAMAMA GROUP kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba ( Eleza hapa habari za madai)**

MADAI YA MKOPO SH. 1,649,000/= Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 24 Mwezi 11 Mwaka 2023 saa 2:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusiskiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 13 Mwezi 11 Mwaka 2023

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO MAFINGA
WILAYA YA MUFINDI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MVOMERO**
**MVOMERO**

**SHAURI LA MIRATHI NA 01 MWAKA 2023**

**KATIKA MIRATHI YA MAREHEMU**
**ANGELUS ENOCK MBILINYI**

**NA**

**KATIKA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI NA**
**HENRY ANGELUS MBILINYI.....................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA JUMLA**
**(Chini ya Kanuni 75 ya Kanuni za Mirathi T.S.Na.369/1963)**

Watu wote wenye kudai kuwa na maslahi katika Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanataarifiwa kuhudhuria kusikilizwa mwenendo wa shauri hili ikiwa wataona vema kabla ya Muombaji aliyetajwa hapo juu hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Ikiwa kuna pingamizi lolote juu ya kuteuliwa kwa muombaji tajwa hapo juu;

Pingamizi liwasilishwe Mahakamani mnamo au kabla ya tarehe 22 Mwezi 11. 2023

Imetolewa Mvomero leo tarehe 20 Mwezi 11/2023

Hakimu Mkazi

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA. 14 YA MWAKA 2023**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**
**ESTOMIHI MOSES MFANGAVO..................MAREHEMU**
**SIRIELI ESTOMIHI MOSES.....................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya terehe 04 Mwezi DISEMBA, Mwaka 2023.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 21 Mwezi NOVEMBA Mwaka 2023.

HAKIMU MKAZI

MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0745 700 710.***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Israel yafunga ubalozi wake Afrika Kusini

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

ISRAEL imefunga ubalozi wake na kumrudisha balozi wake wa Afrika Kusini Eliav Belotserkovsky kwa mashauriano kabla ya kura ya wabunge kuamua hatma ya ubalozi wa Israel nchini humo.

Hayo yanajiri kabla ya kupigwa kura katika bunge la Afrika Kusini kuhusu hoja ya kuufunga ubalozi wa Israel na kukata uhusiano wote na taifa hilo hadi pale usitishaji vita utakapotekelezwa huko ukanda wa Gaza.

Aidha, uhusiano wa kidiplomasia wa nchi hizo mbili hivi karibuni umeshuhudiwa kuongezeka kutokana na vita vya Israel dhidi ya Gaza.

Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa hapo awali alisema nchi yake inaamini kuwa Israel inafanya uhalifu wa kivita na mauaji ya halaiki huko Gaza, ambako maelfu ya Wapalestina wameuawa.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Israel ilichapisha ujumbe kwenye mtandao wa X, (zamani Twitter), ikisema "Kufuatia taarifa za hivi punde za Afrika Kusini, Balozi wa Israel mjini Pretoria ameitwa tena Jerusalem kwa mashauriano".

Hoja iliyowasilishwa na chama cha upinzani cha mrengo wa kushoto cha 'Economic Freedom Fighters' (EFF) inaungwa mkono na chama tawala cha 'African National Congress' (ANC) na vyama vingine vidogo.

Afrika Kusini ilitangaza siku chache zilizopita kwamba imepeleka kile ilichokiita mauaji ya halaiki ya Israel huko Gaza kwa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) kwa uchunguzi, huku baraza lake la mawaziri likiitaka mahakama hiyo kutoa hati ya kukamatwa kwa Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu.

Waziri wa Afrika Kusini katika ofisi ya rais, Khumbudzo Ntshavheni, alisema.

"Kwa kuzingatia kwamba sehemu kubwa ya jumuiya ya kimataifa inashuhudia kutendeka kwa uhalifu huu kwa wakati, ikiwa ni pamoja na kauli ya dhamira ya mauaji ya kimbari ya viongozi wengi wa Israel, tunatarajia kwamba hati za kukamatwa kwa viongozi hao akiwemo Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu, zitolewe hivi karibuni".

Mapema mwezi huu, Afrika Kusini ilimwita balozi wake nchini Israel na kuwaondoa wafanyakazi wake wote wa kidiplomasia nchini humo.

Inalezwa kuwa mzozo huo pia utakuwa mada ya mkutano wa kawaida wa nchi za BRICS, ambao utahudhuriwa na viongozi wa umoja huo, akiwemo Ramaphosa, Rais wa Russia Vladimir Putin na Rais wa China Xi Jinping.

Jumuiya hiyo ya kiuchumi iliundwa na Brazil, Russia, India na China mwaka 2009 na kuongezwa Afrika Kusini mwaka 2010. Iran, Saudi Arabia na Umoja wa Falme za Kiarabu, Argentina, Misri na Ethiopia pia zimepangwa kuingia BRICS.

**HAMAS**

Kiongozi wa Hamas Ismail Haniyeh, alisema kundi hilo limetoa majibu yake kwa Qatar inayosimama kama mpatanishi kati ya pande hizo mbili, na kwamba wanakaribia kufikia makubaliano ya usitishaji vita licha ya kuwa Israel hadi sasa haijatoa kauli yoyote.

Hatua hiyo inajiri baada ya ofisa mkuu wa Marekani kusema kwamba mpango wa kuwaachilia mateka waliochukuliwa kutoka Israel wakati wa mashambulizi ya Hamas mwezi uliopita baada ya kusitisha mapigano, uko karibu zaidi kuliko hapo awali. **BBC**

## Kaya 80,000 zaathiriwa na mafuriko Kenya

**NAIROBI,** KENYA

TAKRIBAN kaya 80,000 zimeathirika kutokana na mvua ya El-Nino inayonyesha nchini Kenya wakati idadi ya kaunti zilizoathirika ikiongezeka hadi 33.

Ilielezwa kuwa mojawapo ya maeneo yaliyoathirika zaidi na mafuriko ni Nyando Kisumu ambako zaidi ya kaya 500 zimelazimika kutafuta hifadhi maeneo salama yenye miinuko huku vijiji vya Ombaka, Kaloo, Kasiwindi Kusini, Kanyipula na Tura vikifurika maji baada ya mto Nyando kuvunja kingo zake.

Licha ya waathiriwa wa Nyando kulalamikia kutopokea msaada wowote tangu walipohamishiwa sehemu salama wiki mbili zilizopita, Gavana wa jimbo la Mombasa Abdull Nassir, alisema serikali yake haijapokea mgao wowote wa pesa kutoka serikalini ili kupambana na janga la mvua huku takriban watu 3,800 wakiripotiwa kuathirika.

Maeneo mengine yaliyoathirika ni pamoja na Kwale ambako miili ya watu watatu iliopolewa katika mto Ramisi baada ya kusombwa na mafuriko, huku Turkana miundombinu ya barabara ikiharibiwa na mafuriko.

Shirika la utabiri wa hali ya hewa lilionya kuwa, maeneo ya Kaskazini na Pwani ya Kenya yatapokea mvua nyingi zaidi ikifuatiwa na Nairobi na eneo la Kati huku takwimu za shirika la Msalaba Mwekundu likisajili vifo vya watu 61, 235 kujeruhiwa na nane hawajulikani waliko.

Takwimu za shirika la Msalaba Mwekundu za tangu mwezi Oktoba mwaka huu zimesajili uharibifu wa biashara 1,143, shule 10 na mifugo 11,610 imeangamia. **DW**





Rais Felix Tshisekedi akiendelea na kampeni za uchaguzi mkuu huko DRC. **PICHA: MTANDAO**.

# Kampeni za uchaguzi zazidi kushamiri DRC

**KINSHASA,** DRC

KAMPENI za uchaguzi mkuu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zimeendelea kushamiri baada ya kinara mwingine wa upinzani Moise Katumbi kuzindua rasmi kampeni zake za kuwania urais wakati akiendelea kupata uungwaji mkono na wagombea wengine.

Aidha, baada ya waziri mkuu wa zamani Matata Ponyo kujiondoa kama mgombea na kutangaza kumuunga mkono Katumbi, wagombea wengine Seth Kikuni na Frank Diongo nao wamefuata mkondo huo.

Wagombea wengine waliozindua kampeni zao ni pamoja na daktari Denis Mukwege na mwanamke pekee kwenye kinyang'anyiro hicho, Marie-Josee Ifoku, ambao wote wameahidi kupambana na vitendo vya rushwa na hali ya usalama ikiwa watachaguliwa.

Akizungumzia juu ya muungano wa wagombea hao, Mchambuzi wa Siasa, Francois Alwende, alisema "Wapinzani wakitaka kupambana na rais Tshisekedi lazima waungane lakini kuungana kwao sio jambo rahisi pia".

Rais wa sasa Felix Tshisekedi anayewania kuchaguliwa kwa muhula wa pili, alizindua kampeni zake jijini Kinshasa kwenye uwanja wa Martyrs, ambako aliahidi kukamilisha ahadi za uchaguzi na kusimamia usalama mashariki mwa nchi hiyo.

Mwingine aliyezindua kampeni zake ni Martin Fayulu, ambaye alikuwa kwenye mji wa Bandundu, alikoahidi raia kuwa atashughulikia changamoto zinazoikabili nchi kwa sasa, huku muwaniaji mwingine Delly Sesanga, akianza kampeni zake katika mkoa wa Kwango, wakati Seth Kikuni na Jean-Claude Baende wakianza kampeni yao huko Kinshasa.

Inaelezwa kuwa ni kampeni zinazotazamwa si tu na raia wa DRC lakini jumuiya ya kimataifa na waangalizi wa uchaguzi, ambao wametoa wito wa amani licha ya eneo la mashariki kukabiliwa na utovu wa usalama, hali inayozua maswali ikiwa baadhi ya maeneo ya mashariki mwa nchi hiyo yatafanya uchaguzi.

**RFI**

# MALIMA AAHIDI LAKI MBILI KILA BAO MTIBWA KUINUSURU ISISHUKE DARAJA

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kile kinachoonesha ni mkakati wa kuinusuru timu ya Mtibwa Sugar, isiendelee kufanya vibaya na kuifanya kuwa kwenye hatari ya kushuka daraja, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, ameahidi kutoa kiasi cha Sh. 200,000 kwa kila bao kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo itaibuka na ushindi.

Mtibwa inaburuza mkia mpaka kufikia raundi ya tisa ya Ligi Kuu, ikiwa na pointi tano, ikishinda mechi moja, sare mbili na kupoteza michezo sita.

Malima alitoa ahadi hiyo juzi alipotembelea kambi ya timu hiyo iliyopo Turiani, mkoani Morogoro na kuongea na uongozi, benchi la ufundi na wachezaji ili kufahamu tatizo linaloikabili kiasi cha kushindwa kufanya vema mpaka sasa.

Mkuu wa Mkoa huyo alikuwa ameambatana na viongozi wa soka mkoani humo, ambapo pamoja na mambo mengine amesema ni aibu kama Mtibwa Sugar itashuka daraja.

"Mtibwa Sugar ndiyo sura ya soka la Morogoro, kama ikishuka ni aibu kubwa kwa hiyo, serikali ya mkoa na wadau wa soka sisi wote tufanye kila linalowezekana kuisimamia timu hii, kukuza hamasa kwa ajili ya kuhakikisha haishuki," alisema Mkuu wa Mkoa huyo kwenye ziara hiyo ya kurejesha hamasa.

Mwenyekiti wa Chama cha Soka Mkoa wa Morogoro, Paschal Kihanga, alisema walichokibaini ni kukosekana kwa umoja kwa viongozi na hata miongoni mwa wachezaji.

"Tumeambiwa kuna mgawanyiko, kwa hiyo sasa tunataka kuwaunganisha tuwe kitu kimoja, hii itasaidia wote kuongea lugha moja," alisema.

Nahodha wa kikosi hicho, Oscar Masai, alikiri kuwa kuna msuguano ndani ya klabu hali inayosababisha mambo kutokwenda sawa.

"Ni kweli kuna vitu vilikuwa haviendi sawa, lakini kwa ujio wa mkuu wa mkoa ameweka mambo sawa, timu itaenda vizuri," alisema nahodha huyo.

Kocha Mkuu, Zuberi Katwila, alisema kwa sasa wapo kwenye mkakati wa kuiweka timu kwenye mstari ambao Mtibwa Sugar imezoeleka kuwa.



Timu nne za Safari Lager Cup kutoka mikoa minne. Juu kushoto ni timu ya Mwanza, Dar es Salaam (juu kulia), Arusha (chini kushoto) na Mbeya (chini kulia). **MPIGAPICHA WETU**

# Timu za Safari Lager Cup zatangazwa rasmi

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya Safari Lager Cup yanayodhaminiwa na Bia ya Safari Lager, yamezidi kunoga huku timu zikiwa tayari zimetangazwa.

Msemaji wa mashindano hayo, yaliyoleta msisimko wa aina yake, Mbwiga Mbwiguke, alisema zoezi hilo la kuibua vipaji, liliendeshwa kwa ukamilifu kama ilivyopangwa na tayari wachezaji 22 kutoka kila mkoa wameshachaguliwa.

"Kama tulivyowaarifu hapo awali, zoezi hili lilishirikisha mikoa ya Mbeya, Mwanza, Arusha na hatimaye Dar es Salaam, ambapo makocha mahiri, Jamhuri Kihwelo na Sekilojo Chambua, walikuwa na kazi ngumu ya kuchagua kikosi cha wachezaji 22 kutokana na mabonanza mbalimbali waliyoshiriki baada ya usajili," alisema.

Alisema hatua inayofuata sasa ni timu hizo nne kushindanishwa na kisha makocha watachagua timu moja itakayojulikana kama Safari Lager Champions ambayo hatimaye itacheza na timu mojawapo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Meneja wa Bia ya Safari Lager, Pamela Kikuli, aliwapongeza makocha Jamhuri Kihwelo na Sekojo Chambua kwa kuendesha zoezi hilo kwa weledi mkubwa na kutumia uzoefu wao kuchagua timu hizo.

Alisema Bia ya Safari, ambayo ni ya mabingwa iliamua kuja na kampeni hiyo ili kuibua vipaji vipya kabisa vya mpira wa miguu kwani wanaamini kuna vipaji vingi nchini ambavyo havijaibuliwa.

Aliongeza kuwa hatua inayofuata itakuwa na msisimko mkubwa kwani timu nne zilizochaguliwa zitachuana ili kupata timu moja ya wachezaji 22 itakayocheza na timu ya Ligi Kuu.

Kocha Kihwelo alisema zoezi limefanikiwa kwa asilimia 90 hasa ikizingatiwa kuwa ndio mara ya kwanza na waliojitokeza walikuwa wengi zaidi na wao kama makocha walikuwa na kibarua kigumu cha kuchuja kwani katika mikoa yote minne kulikuwa na vipaji vya kipekee.

"Sio kwamba walioachwa ni wabaya, ni kwamba tu walihitajika 22, lakini kiwango cha vipaji kiko juu na tunaishukuru Safari Lager kwa kuona umuhimu wa kuibua vipaji vya mpira wa miguu kwani wengi walikuwa wanakosa nafasi ya kutoka," alisema na kutoa wito kwa klabu mbalimbali zenye programu ya U-20 kuwatumia vijana walioachwa kwa kuwa wana vipaji vya hali ya juu.

Kocha Chambua alisema zoezi hilo lilikuwa la aina yake kwani limedhihirisha kuwa kuna vipaji vya hali ya juu katika mikoa mbalimbali na kutoa wito kwa kampuni nyingine ziige mfano wa Safari Lager kwa kutenga fedha na rasilimali kwa ajili ya kuibua na kukuza vipaji.

"Zoezi lilikuwa gumu maana kuna vipaji vya hali ya juu. Tulitamani tuwachukue wote, lakini nafasi zilikuwa 22 tu kwa kila mkoa. Tumearifiwa kuwa zoezi hili ni endelevu kwa hiyo tunaamini mwakani litakuwa kubwa zaidi ili Safari Lager iendelee kuibua vipaji zaidi.

Bia ya Safari Lager imewahi kudhamini mashindano ya Taifa Cup ambayo yalishirikisha mikoa yote ya Tanzania kwa lengo la kuibua vipaji.

## BMT yawatuma kombe Kuogelea

**Na Shufaa Lyimo**

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limewataka wachezaji wa timu ya Taifa ya mchezo wa Kuogelea kuhakikisha wanakwenda kufanya vizuri na kuutetea ubingwa wao kwenye mashindano ya nane ya African Aquatics kanda ya 3, yatakayoanza kutimua vumbi Novemba 23 - 25, mwaka huu, Kigali nchini Rwanda.

Akizungumza jiijini Dar es Salaam jana, wakati akikabidhi bendera kwa timu hiyo, ambayo imeondoka jana kuelekea Rwanda, Katibu Mtendaji wa BMT, Neema Msitha, aliwataka wachezaji hao kwenda kuipeperusha vema bendera ya Tanzania kupitia mashindano hayo.

"Serikali ipo nyuma yenu, tunaamini mtakwenda kuutetea ubingwa wenu kutokana na maandalizi ya muda mrefu mliyoyafanya ili mtakaporudi tuje kuwapokea kwa furaha," alisema Msitha.

Aidha, aliwapongeza viongozi wa Chama cha Mchezo wa Kuogelea Tanzania (TSA), kutokana na jitihada wanazozifanya ikiwamo kuandaa mashindano ya mara kwa mara yenye lengo la kuinua vipaji vya vijana.

## KVZ yanyukwa, kocha atoa neno

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya KVZ FC imeendelea kurejeshwa nyuma katika harakati zake za mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya hapo juzi kuchezea kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Jamhuri SC kutokea Kisiwani Pemba.

Mchezo huo wa mzunguko wa 12 ulichezwa katika Uwanja wa Mau A huku bao pekee lililowapa alama tatu Jamhuri SC likifungwa na Suleiman Massoud dakika ya 59.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Maafande hao wa KVZ FC, Ali Mohmed Ameir, alisema wapinzani wao, Jamhuri SC walikuja wamejipanga kwa ajili ya kupata ushindi ugenini baada ya kutofanya vizuri michezo miwili waliyocheza wakiwa Unguja.

Alisema kulingana na msimamo wa ligi hiyo, Jamhuri walicheza kwa ari kubwa na kufanikiwa kupata bao ambalo walilinda mpaka dakika ya 90.

Alisema mara nyingi unapokutana na timu ambayo ipo katika nafasi za chini kwenye msimamo wa ligi, hucheza vizuri na kwa ari kubwa ili kupata matokeo mazuri na kulinda goli iwapo watatangulia kufunga na ndicho kilichotokea.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**TONEY FEDHA NYINGI**

CHELSEA inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27, kwa fedha nyingi katika kipindi cha dirisha la usajili la Januari. **(Football.London)**

**KVARATSKHELIA AWINDWA**

CHELSEA, Manchester City, Manchester United na Newcastle United zote zilituma wawakilishi kumtazama winga wa Napoli, Khvicha Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 22, wakati wakishindwa kwao kwa mabao 3-1 na Hispania Jumapili. **(90min)**

**LEONARDO ANYATIWA ARSENAL**

ARSENAL na Manchester United ni miongoni mwa klabu zinazotarajiwa kuonesha nia ya kumnunua mshambuliaji wa Brazil, Marcos Leonardo mwenye umri wa miaka 20, ambaye wakala wake anasema atataka kuondoka Santos Januari. (Evening Standard)

**MBAPPE KUZUNGUMZIA MKATABA**

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24, amesema "kutakuwa na wakati wa kuzungumza" kuhusu mustakabali wake pale Paris St-Germain anapojiandaa kuingia miezi ya mwisho ya mkataba wake na klabu hiyo ya Ligue 1. **(Telefoot, via Mail)**

**NEVES AWEKEWA NGUMU**

KLABU ya Benfica haina mpango wa kuingia kwenye mazungumzo juu ya kiungo wa kati wa Ureno, Joao Neves mwenye umri wa miaka 19, ambaye amekuwa akifuatiliwa na Manchester United, akiwa na kipengele cha kuuzwa cha pauni milioni 105. **(Fabrizio Romano)**

**VARANE ATAKIWA BAYERN**

KLABU ya Bayern Munich inaweza kufikiria kumnunua beki wa kati wa Manchester United na Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 30. **(Sky Germany)**

**LIVERPOOL KUMZUIA DIAZ**

LIVERPOOL haitakubali ofa kwa winga wa Colombia, Luis Diaz mwenye umri wa miaka 26, licha ya ripoti nchini Hispania kwamba wanaweza kuidhinisha makubaliano ya kubadilishana na Barcelona kumnunua mshambuliaji wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 26. **(Football Insider)**

**ALONSO NA LEVERKUSEN**

KOCHA wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso, hana kipengele cha kuuzwa katika mkataba wake kinachomruhusu kujiunga na moja ya timu zake za zamani, Mkurugenzi Mtendaji wa klabu hiyo amesema, huku kukiwa na ripoti kwamba raia huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 41 anaweza kuhamia Liverpool, Real Madrid au Bayern Munich. (Talksport)

**CRISTANTE KUTUA SPURS**

KLABU ya Tottenham Hotspur iko tayari kuwapa AS Roma pauni milioni 26 kwa ajili ya kiungo wa kati wa Italia, Bryan Cristante, 28. **(Tuttomercatoweb, via Teamtalk)**

**RICHARLISON NA TOTTENHAM**

TOTTENHAM Hotspur haijafurahishwa na madai ya Everton kwamba kukataa kwao kulipa pauni milioni 80 kumnunua mshambuliaji wa Brazil, Richarlison mwenye umri wa miaka 26 kulisababisha 'The Toffees' hao kukiuka kanuni za matumizi ya fedha za Ligi Kuu England. **(Mail)**

## DON ZA SOKA
## MAGA A ULAYA




# JEZI YA MESSI YA KOMBE DUNIA KUUZWA MABILIONI

### Itaipiku ile ya Maradona bao la 'Mkono wa Mungu' iliyopigwa bei kwa Sh. bilioni 21...

**NEW YORK, Marekani**

JOZI tatu tofauti za jezi zilizovaliwa na nahodha wa Argentina, Lionel Messi, wakati wa michuano ya Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar, zitauzwa kwa njia ya mnada.

Messi mwenye umri wa miaka 36, alifanikiwa kutwaa Kombe la Dunia akiwa na Argentina katika michuano hiyo mwaka jana.

Messi alicheza katika mechi zote saba za michuano hiyo, lakini jezi mbili pekee kati ya tatu ambazo Messi alivaa wakati wa hatua ya makundi ndizo zitakazouzwa kwenye mnada, baada ya mchezaji wa Australia, Cameron Devlin, kubadilishana na mshambuliaji huyo wa zamani wa Barcelona wakati wa mchezo baina ya timu hizo.

Jezi iliyovaliwa na mshambuliaji huyo wakati wa mchezo wa fainali dhidi ya Ufaransa inatarajiwa kuuzwa zaidi ya pauni milioni 8 (Sh. bilioni 24.8), katika mnada maalum utakaoendeshwa na Kampuni ya Sotheby jijini New York, Marekani.

Rekodi pekee ya mauzo ya jezi ya Argentina iliopo kwa sasa ni ile iliyowekwa baada ya mauzo ya gwiji wa soka wa nchi hiyo, Diego Maradona, ambayo aliivaa kwenye mchezo dhidi ya England mwaka 1986 na kufunga bao la mkono wa Mungu.

Jezi ya Maradona ilipigwa mnada mwaka 2022 kwa mauzo ya pauni milioni 7.1 (Sh. bilioni 21.7).

Kiongozi Mkuu wa Kampuni ya mnada ya Sotheby, Brahm Wachter amesema uuzaji wa jezi ya Messi "unasimama kama tukio kubwa katika historia ya mnada."

"Kombe la Dunia la FIFA la 2022 linasimama kama moja ya matukio makubwa zaidi katika historia ya michezo, yanayohusiana sana na safari ya ushujaa ya Messi na kuweka hadhi yake kama mchezaji bora zaidi wa wakati wote," alisema Wachter.

Messi ambaye ni mshindi mara nane wa Ballon d'Or, amekuwa mchezaji wa kwanza katika historia ya Kombe la Dunia kufunga katika hatua ya makundi, 16-bora, Robo Fainali, Nusu Fainali na Fainali ya michuano hiyo.

Jezi za Messi zitaonekana katika makao makuu ya Sotheby jijini New York katika maonesho ya bure ya umma wakati wa mchakato wa zabuni, ambayo itafunguliwa kati ya Novemba 30 na Desemba 14, mwaka huu.

# VINICIUS JR KURUDI DIMBANI FEBRUARI

**SAO PAULO, Brazil**

KIUNGO mshambuliaji wa Brazil na Klabu ya Real Madrid, Vinicius Jr, anatarajiwa kurejea uwanjani Februari mwakani baada ya kuumia kwenye mechi ya kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Colombia.

Vinicius Jr alishindwa kuendelea na mchezo huo uliopigwa mwishoni mwa wiki iliyopita na kutolewa nje akiwa anachechemea, hali ambayo ilisababisha kuzusha hofu kwa mashabiki wa Real Madrid.

Kabla ya kuumia kiungo huyo alitengeneza nafasi ya bao lililowekwa kimiani na Gabriel Martinelli dakika ya nne, lakini alishindwa kuendelea na mchezo kutokana na jeraha alilopata, nafasi yake ikichukuliwa na Joao Pedro.

Vinicius Jr mwenye umri wa miaka 23, amekuwa akikabiliwa na tatizo la maumivu ya misuli ya paja msimu huu wa 2023/24, huku maumivu mengine sehemu ya paja yakiibuka.

Baada ya mchezo kumalizika Vinicius alisema: "Jeraha hili linafanana na lile lililopita, nilikuwa na uvimbe ndio mana nikasikia maumivu."

Sasa taarifa imethibitisha kuwa Vinicius aliondolewa kwenye kikosi cha Brazil ambacho jana Jumatano kilikuwa kinacheza na Argentina.

Kuumia kwa mchezaji huyo ni pigo kwa Real Madrid, kwani inakabiliwa na wachezaji wengi majeruhi wa kikosi cha kwanza na hivi karibuni kiungo wa timu hiyo, Eduardo Camavinga, aliumia akiwa katika majukumu ya kimataifa na Timu ya Taifa ya Ufaransa.



# Mendy sasa adai mishahara yake City



**MANCHESTER, England**

BENJAMIN Mendy amewasilisha madai ya mamilioni ya pauni dhidi ya klabu yake ya zamani ya Manchester City kuhusu mishahara ambayo haijalipwa, wakili wake ameithibitishia ESPN.

Mendy mwenye umri wa miaka 29, hakukutwa na kosa kwenye kesi ya ubakaji iliyosikilizwa Julai.

Hiyo ni baada ya kufunguliwa kesi ya makosa sita ya ubakaji aliyotuhumiwa nayo na shtaka moja la unyanyasaji wa kingono Januari.

Mashtaka dhidi ya Mendy yaliifanya Man City kumsimamisha beki huyo Agosti, 2021 kabla ya hatimaye kusitisha malipo yake Septemba 2021.

Beki huyo alisajiliwa na Lorient ya Ligue 1 kwa uhamisho wa bure msimu huu wa majira ya joto baada ya kumalizika kwa mkataba wake na Man City.

Nick De Marco KC, ambaye anasimamia kesi kwa niaba ya Mendy, alithibitishia ESPN kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa amewasilisha madai ya pauni milioni nyingi kwa kukatwa kwa mishahara bila kibali kwenye Mahakama ya Ajira.

"Manchester City FC ilishindwa kumlipa Mendy ujira wowote kuanzia Septemba 2021 hadi Juni 2023 baada ya kushtakiwa kwa makosa mbalimbali ambapo yote hakukutwa na hatia na aliachiwa huru.

Madai hayo yatawasilishwa mbele ya Mahakama ya Ajira," alisema katika taarifa iliyotumwa kwa barua pepe kwa Reuters.

Mendy, ambaye alisajiliwa na Man City kutoka Monaco mwaka 2017, alichezea klabu hiyo ya Ligi Kuu mara 75 na kushinda mataji matatu katika muda wake huko. Mechi yake ya mwisho akiwa na City ilikuwa dhidi ya Tottenham Hotspur Agosti, 2021.

Hata hivyo, Man City ilikataa kuzungumzia lolote ilipoulizwa na Reuters.

# Juventus yanogewa na Chiesa

**TURIN, Italia**

KLABU ya Juventus inapanga kufanya mazungumzo ya kuongeza mkataba mpya kwa mshambuliaji na mchezaji wa kimataifa wa Italia, Federico Chiesa, katika wiki zijazo, kwa mujibu wa ESPN.


Mchezaji huyo wa zamani wa Fiorentina, ambaye 'Bianconieri' walimlipa ada ya euro milioni 50 pamoja na bonasi katika msimu wa majira ya joto wa 2020, ana mkataba hadi msimu wa majira ya joto wa 2025, lakini kuna hatari ya kuondoka bure ikiwa mkataba mpya hautakubaliwa hapo awali msimu ujao.

Kwa mujibu wa taarifa ya Juventus kupitia ESPN, tayari wamekuwa kwenye mazungumzo na Chiesa kuhusu kuongezwa mkataba upya, lakini hawakuweza kukamilisha rasmi mkataba mpya katika majira ya joto.

Juventus wana nia ya kumbakiza Chiesa, taarifa zaidi ni kwamba klabu hiyo inaweza kutoa nyongeza ya mkataba wa muda mfupi hadi msimu wa majira ya joto wa 2026 ili kuziba pengo hilo kwa msimu mwingine.

Imeripotiwa kuwa Chiesa atapewa mshahara ule ule anaopata sasa, kiasi cha euro milioni tano kwa msimu, na uwezekano wa kujadili nyongeza katika siku zijazo.

Chiesa amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi tangu kujiunga na Juventus huku pia aking'ara katika kikosi cha Timu ya Taifa ya Italia.



HABARI MICHEZO

# PRISONS KUMTANGAZA MRITHI WA MINZIRO LEO

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Tanzania Prisons umesema upo kwenye mchakato wa kutafuta Kocha Mkuu ambaye wanatarajia kumtambulisha muda wowote kuanzia leo baada ya kufikia makubaliano ya pande zote mbili.

Hatua hiyo ya kutafuta kocha mpya ni baada ya kuvunja mkataba na Felix Minziro kutokana na mwenendo mbaya wa timu hiyo katika michezo yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa nafasi ya 14 wakikusanya alama saba kwenye msimamo.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Tanzania Prisons, Ajabu Kifukwe, alisema Bodi ya Wakurugenzi ya timu hiyo tayari imeanza mchakato wa kutafuta kocha mkuu haraka.

Alisema wameangalia vigezo vyao ikiwamo kupata kocha mzawa ambaye atachukua nafasi ya Minziro kwa lengo la kukisuka kikosi cha timu hiyo ili kufikia malengo yao.

"Tunechukuwa maamuzi mapema ya kutafuta kocha mkuu mwingine baada ya kuachana na Minziro ambaye hakuwa na upepo mzuri katika huu msimu, mchakato uko vizuri na muda wowote kuanzia sasa tutamtangaza kocha mpya," alisema Kifukwe.

Aliongeza kuwa wanatarajia kocha huyo kupatikana kwa haraka kabla ya Alhamisi ambapo watakuwa na mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Coastal Union.

Tanzania Prisons itakuwa na mchezo wake wa ligi Alhamisi hii, wakiwa katika uwanja wa nyumbani, Sokoine jijini Mbeya, kuwakaribisha Coastal Union.



Mkurugenzi wa Bendi ya Extra Bongo, Ally Choki, akitangaza ujio wa bendi hiyo, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni mratibu wa shughuli za bendi hiyo, Juma Kasesa na Meneja wa Andrew's Lounge, Kalumbi Seleman. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Exra Bongo rasmi sasa Extra Bongo Baba Lao

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI nyota wa Muziki wa Dansi nchini, Ally Choki, amesema bendi yake ya Extra Bongo ambayo imeifufua upya, sasa itakuwa inaitwa Extra Bongo Baba Lao.

Choki alisema hayo wakati alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana akitangaza rasmi ujio wa bendi hiyo.

"Ni Baba Lao kwa sababu ninaamini itakuwa Bora zaidi kuliko Extra Bongo ya kwanza na ya pili, hivyo nimejipanga vizuri kuhakikisha inasimama imara," alisema Choki.

Alifafanua kuwa awali bendi hiyo ilijulikana kama Extra Bongo Wazee wa Kujinafasi, na kwamba wamehama kutoka jina hilo hadi Baba Lao, kwa kuwa wanataka kuleta upinzani katika muziki wa dansi.

"Lakini pia ni Extra Bongo Baba Lao kwani inaundwa na damu mchanganyiko, nyingi zikiwa changa na wakongwe wachache," alisema.

Bila kutaja jina, Choki alisema atakwenda kunyofoa wanamuziki wawili kutoka bendi kubwa za jijini Dar es Salaam ili kukamilisha kikosi chake ambacho kitakuwa na wanamuziki wasiopungua 15.

Bendi ya Extra Bongo ilikufa mwaka 2015 na sasa Choki anasema amejiandaa ili asifanye makosa ambayo yatasababisha ife tena, kwa maelezo kwamba miaka yote ambayo amekaa bila Extra Bongo, amejifunza mengi ya kumfanya asimame imara.

## Yanga yaifuata Belouizdad na mkakati mkali

INATOKA UK. 24

"Tutakuwa makini sana, baada ya hapo tutarudi Dar es Salaam kucheza dhidi ya Al Ahly Desemba 2. Hii yote miwili nadhani ndiyo dira ya nini tufanye msimu huu kwenye hatua ya makundi," alisema Kamwe.

Akizungumzia kuhusu kuondoka kwa mafungu, alisema kundi la kwanza lililoondoka ni la wachezaji ambao hawakuitwa na timu ya taifa, lakini litakalofuata ni la wachezaji ambao walikuwa wakizitumikia timu za taifa na hasa Taifa Stars.

"Tunaondoka fungu la kwanza, hawa ni wachezaji ambao hawakuitwa kwenye timu zao za taifa, walikuwa wanaendelea na mazoezi, kundi la pili litaondoka kesho (leo), baada ya majukumu ya timu za taifa na kama unavyofahamu, kundi kubwa la wachezaji wa Yanga wapo kwenye kikosi cha timu ya taifa, mwalimu alikuwa anaangalia zaidi wachezaji kuhusu utimamu wao wa mwili.

"Hata waliokuwa kwenye majukumu mengine alikuwa akiwasisitiza kuhusu kutunza fiziki zao kwa sababu ndiyo msingi mkubwa wa mchezaji kufanya vema, lengo ni kweli kucheza soka zuri na kupata ushindi kule Algeria," alisema Kamwe.

Mechi dhidi ya CR Belouizdad itakuwa ni ya kwanza kwa Yanga Ligi ya Mabingwa hatua ya makundi baada ya miaka 25, kwani mechi yao ya ufunguzi mwaka 1998 ilicheza dhidi ya Manning Rangers ya Afrika Kusini, Agosti 22, Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam (sasa Uhuru), ikitoa sare ya bao 1-1.

Mara ya mwisho kucheza mechi ya hatua ya makundi ilikuwa ni Novemba 8, mwaka 1998, ikibamizwa mabao 3-0 dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, jijini Dar es Salaam na tangu hapo haijaweza kutinga tena kwenye hatua hiyo hadi mwaka huu.

# Simba warejesha umoja kuiua Asec

INATOKA UK. 24

"Kwa umoja wetu huu, kilichowakuta mwaka jana ndio tunaenda kukifanya hicho Jumamosi, kumfunga Asec Mimosas hapa nyumbani, ndicho kitakachotea katika uwanja kwa mara nyingine," alisema Ahmed.

Kwa upande wa mashabiki wa Simba, akiwamo Justine Mwakitarima, amewataka Wanasimba wenzao kujitokeza kwa wingi uwanjani kusapoti timu yao na kuendeleza ubora wao ambao hivi karibuni Shirikisho la Soka duniani (Fifa), walitoa tuzo bora kwa mashabiki wa Wekundu Msimbazi.

"Twendeni kwenye uwanja kwa wingi ili kuwa sehemu ya kuwapa hamasa wachezaji wetu kupambania klabu Jumamosi dhidi ya Asec Mimosas," alisema.

Alisisitiza kuwa wanatakiwa kusahau yote yaliyopita nyuma na sasa nguvu na akili zao iwe kwenda kwa wingi Uwanja wa Benjamin Mkapa ili kuonesha kile ambacho walitunukiwa na Fifa kuwa Simba ni mashabiki bora. Februari 13, mwaka 2022, Simba iliwafunga Asec Mimosas mabao 3-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa ukiwa ni mchezo wa Kundi D wa Kombe la Shirikisho Afrika .

Mabao ya Simba katika mechi hiyo yalifungwa na Pape Sakho dakika ya 12, Shomari Kapombe kwa penalti (dk. 79) na Peter Banda (dk. 81) huku la Asec Mimosas likifungwa na Stephane Aziz Ki dakika ya 60, ambaye kwa sasa anaichezea Yanga. Katika mchezo wa marudiano ugenini Machi 20, 2022 nchini Ivory Coast, Simba ilikubali kipigo cha mabao 3-0, yakifungwa na Aubin Kramo dakika ya 16, ambaye kwa sasa anaitumikia Simba, hata hivyo hatakuwa sehemu ya kikosi kitakachocheza Jumamosi kutokana na kuwa nje akiuguza majeraha.

Mabao mengine katika mechi hiyo yaliyofungwa na Aziz Ki dakika ya 25 na Karim Konate dakika ya 57. Konate kwa sasa anaichezea FC Red Bull Salzburg ya Australia.

# Michezo

Jumatano Novemba 22, 2023


Nipashe



## Jezi ya Messi ya Kombe Dunia kuuzwa bil. 24/-

UKURASA 21

**NGUVU MOJA!...**



Baadhi ya mashabiki wa Simba, wakizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, baada ya uongozi wa klabu hiyo kuwajumuisha katika mkutano na wanahabari ikiwa ni sehemu ya kurejesha hamasa na kaulimbiu yao ya 'Simba Nguvu Moja', kuelekea mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi wiki hii. **MPIGAPICHA WETU**

# YANGA YAIFUATA BELOUIZDAD NA MKAKATI MKALI

●●●Yaenda kwa mafungu, nyota walioko timu za taifa kuifuata leo, yaanika malengo ikisema...

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha kwanza cha Yanga kimeondoka nchini usiku wa kuamkia jana, tayari kwenda kuivaa timu ya Chabab Riadhi de Belouizdad ya Algeria katika mechi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi.

Kikosi cha pili kinatarajia kuondoka leo kwenda kuungana na wenzao kwa ajili ya mechi hiyo ya Kundi D, itakayochezwa keshokutwa, Ijumaa katika Uwanja wa Julai 5, 1962 (Stade du 5 Juillet 1962) jijini Algiers, Algeria.

Akizungumza muda mchache tu kabla ya kukwea pipa kuelekea Algeria, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema wameianza safari hiyo lengo likiwa ni kwenda kuiwakilisha Yanga na Watanzania kwa ujumla katika lengo lao la kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo hata hivyo amesema ni kazi ngumu na lazima wapambane vya kutosha.

"Tunataka kufanya vizuri ili kuwafurahisha wanachama na mashabiki wa Yanga. Tunataka kufanya vizuri msimu huu ili kufika kwenye 'levo' ambayo hakuna timu yoyote ambayo imewahi kufika hapa Tanzania, na hauwezi kufika hapo kama hujafanya vizuri kwenye hatua ya makundi, huu mchezo wa kwanza wa ugenini ni muhimu kwetu sisi kwa sababu unakwenda kutupa mwongozo wa nini tutegemee kwenye mechi zinazofuata.

INAENDELEA UK. 23

# Simba warejesha umoja kuiua Asec

**Na Saada Akida**

BAADA ya Sintofahamu na kutokea mengi ikiwamo mashabiki kuwarushia maneno viongozi, Klabu ya Simba imekuja na mpango mpya wa kuwaweka karibu kutoa kipaumbele kwao katika mambo mbalimbali yanayohusu klabu hususan kuelekea mchezo wao wa Jumamosi wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast.

Hatua hiyo ni baada ya mashabiki na wanachama wa Klabu ya Simba hivi karibuni kuwarushia maneno viongozi wao kutokana na kufungwa mabao 5-1 dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga.

Kuelekea mchezo wao wa Jumamosi dhidi ya Asec Mimosas, viongozi wa Simba wameamua kushikamana na kuhakikisha wanafanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yao hususan mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema dhumuni lao ni kuimarisha kaulimbiu yao ya 'Simba Nguvu Moja' na kusahau yote yaliyopita na sasa kuweka mambo sawa.

Alisema kuelekea mchezo wao wa Jumamosi wanaunganisha nguvu zao na wote kuwa kitu kimoja ili kufanikiwa malengo ya kusaka ushindi dhidi ya Asec Mimosas.

"Mchezo huu unahitaji zaidi mashabiki kuja uwanjani, tunataka kuendeleza utamaduni wa kujaza uwanja. Tumewachukua mashabiki wachache waje kuwaambia wenzao kuja uwanjani. Hivi karibuni tumepata tuzo ya mashabiki bora Afrika, kama klabu tunataka kuwashukuru kwa kazi kubwa," alisema Ahmed.

Aliongeza kuwa wanahitaji kuonesha ukubwa wao kwa kuendelea kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa na katika hilo, lazima waungane na mashabiki wao kuhakikisha wanamfunga Asec Mimosas Uwanja wa Mkapa.

Alisema kulingana na maandalizi ya timu yao wanaimani kubwa wapinzani wao kitawakuta kile walichokipata mwaka jana walipokutana katika uwanja huo.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042